# Nipashe

Jumamosi Mei 9, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580227

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Kujifukiza kulivyopandisha bei limao, vitunguu swaumu


UK. 2




UKURASA 11

# Kigwangalla: Wageni wasiwekwe karantini

**SERIKALI** yataja sababu kutotangaza wagonjwa wapya, yasisitiza corona inaendelea kuua... *UK. 2, 3*



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (kulia), akionyesha sehemu ya shehena ya dawa ya kutibu ugonjwa wa Corona, baada ya kukabidhiwa msaada na Serikali ya nchi ya Madagascar, nchini humo jana. **PICHA: MTANDAO.**

## BAA LA CORONA



Usifanye mazoezi kama una homa, kikohozi au matatizo ya kupumua. Kaa nyumbani upumzike.
WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## UDSM KUUNDA MASHINE YA KUPUMULIA

UKURASA 2

**RIPOTI MAALUM - 6**

## Sheria kulinda ardhi ya kilimo yaja

UK. 4



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** YANGA YAANZISHA MPANGO KAZI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA



Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Abdallah Mtinika (katikati), akikagua vifaa maalumu vya kunawia mikono, vinavyotengenezwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alipotembelea chuoni hapo jana, kuangalia utengenezaji wa barakoa na vitakasa mikono. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri: Wageni wasiwekwe karantini

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, ameiomba serikali kuondoa utaratibu wa wageni kujitenga kwa lazima kwa siku 14 baada ya kuingia nchini, ili kuvutia watalii.

Akijibu hoja mbalimbali za wabunge waliotaka kusikia mpango wa serikali katika kuokoa utalii unaoendelea kudidimia kutokana na janga la corona, alisema ombi jingine ni kufungua mipaka na kuruhusu ndege za kimataifa kuanzia Juni, mwaka huu.

Bunge hili lilijadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2020/21 na kuyapitishwa.

Kwa mujibu wa Kigwangalla, tathmini iliyofanywa inaonyesha sekta ambayo itawahi kukua haraka baada ya milango ya biashara kufunguliwa ni ya utalii.

"Pamoja na habari mbaya tulizonazo, kuna habari njema, itakuwa sekta ya kwanza kuanza kurejea katika hali yake kuliko nyingine," alisema na kuongeza;

"Tumeamua kujipanga vizuri mwezi huu wa Mei, na tumeanza kuomba vibali kwa viongozi wakuu waturuhusu kufanya haueni kwa kuondoa ulazima wa wageni kujitenga (mandatory quarantene) ya siku 14."

"Mtu akija na ndege akatua Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere au KIA anatakiwa kujitenga kwa gharama zake, mtu hawezi kuja kutalii kwamba kwanini aje ajitenge kwa siku 14 kwa gharama zake halafu ndiyo akatalii," alisema.

"Unaona ni sharti ambalo kwa sasa si sawa, tuliliweka wakati tunazuia maambukizo kutoka nje, lakini sasa tuna maambukizo ya ndani na corona tunaishi nayo bungeni na kila sehemu."

Alisema lazima tujifunze kuishi na corona na haiwezekani kuikwepa bali watu warudi kwenye shughuli zao wazalishe na kukuza uchumi kwa sababu hadi sasa vifo vya corona havijafika 100, lakini watu wakikosa chakula kwa miezi mitatu kutakuwa na vingi kuliko vya ugonjwa huo.

"Ni vyema tukatafakari sana jambo hili nasi kwenye sekta ya utalii tunaona nchi zitakapofungua mipaka watu watataka kwenda kupumzika hivyo watataka kusafiri na kwamba Tanzania ianze kuwapokea, ndani ya serikali tunazungumza kuondoa siku za lazima za kujitenga 14 ili iwe rahisi ndege kuja nchini," alisema.

Alisema pia watafungulia ndege za kimataifa kuja nchini na kuanzia Aprili 3, mwaka huu Shirika la Ndege la Emirate, lilianza kufanya safari muhimu kwa malengo fulani ikiwamo kurudisha watu kwao.

Waziri Kigwangalla alisema Mei 3, mwaka huu, Shirika la Ndege la KLM lilianza safari zake, na leo (Mei 8) Shirika la Ndege la Swiss linafungua safari zake na wamesha gundua corona ipo ni lazima kuishi nayo.

**KIKAO CHA WADAU**

Alisema Wizara imeitisha kikao Jumatatu cha wadau wa utalii kujadili namna ya kuendelea na biashara hiyo wakati huu wa corona kuanzia Juni, mwaka huu.

"Kama mashirika makubwa ya ndege yameanza safari, hoteli ni lazima tukae tayari kuanza biashara mwezi Juni, tutatengeneza mwongozo wa usalama kwa ujumla na kuweka masharti ya lazima kwenye kuvaa barakoa, usafi, namna ya kusafisha vyumba na usafiri ili kuwahakikishia wakija kutalii wawe salama," alisema.

**AOMBA AHUENI YA KODI**

Alisema amewasilisha serikalini maombi ya kuwapa ahueni ya kodi, riba za mikopo na kodi za kisheria kwa wafanyabiashara wa sekta hiyo.

Waziri Kigwangalla alisema wameweka mapendekezo ya kikodi kwa kuwa makadirio hufanyika Januari kwa robo zote nne na wanatakiwa kulipa robo ya kwanza Machi 31. "Wakati anakadiriwa kodi kulikuwa hakuna vikwazo vya kusafiri wala zuio lolote, alikuwa na uhakika wa wageni lakini leo wageni wameahirisha na makadirio aliyoyafanya hayatapatikana,"alisema na kuongeza;

"Tukiendelea kumbana alipe kodi maana yake atafunga biashara na kutangaza kufilisika na kuondoa wafanyakazi na madhara ya kiuchumi na kijamii, ndiyo maana tumeona ni jambo muhimu tulipendekeze kwa wenzetu (Wizara ya Fedha) waone namna ya kufanya ili tupate ridhaa ya serikali ili wafanyabiashara wa utalii wapate ahueni," alisema.

Alisema corona itakapoisha na kufunguliwa kwa biashara ya utalii ni lazima kutoa msamaha wa kodi za kutua, uegeshaji wa ndege na kutakuwa na ushindani wa mashirika ya ndege, hivyo inatakiwa kutangaza mapema ahueni ya kodi kwa watu wa usafirishaji wa anga.

"Mapendekezo mengine ni riba za mikopo kwa wafanyabiashara wenye mikopo kwa Hazina kutoa ahueni kwa kuahirisha baadhi ya riba za mikopo na malipo ya kisheria kama kodi ya mshahara (PAYE) na nyinginezo ili mtu asidaiwe wakati huu ambao hatengenezi fedha," alisema.

# Malimao, vitunguu swaumu bei juu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imesema mabadiliko ya fahirisi za bei ndani ya miezi miwili yameongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya baadhi ya bidhaa ikiwamo malimao na vitunguu swaumu ambazo zinatumika kujifukiza kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Hata hivyo, alisema mfumuko wa bei kwa mwezi Aprili 2020, umepungua hadi asilimia 3.3 kutoka asilimia 3.4 kwa mwaka ulioishia mwezi Machi, 2020.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya watu na takwimu za jamii wa ofisi hiyo, Ruth Minja, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya mfumuko wa bei nchini.

Alisema kwa kipindi kati ya Machi na Aprili, 2020, fahirisi za bei zimeongezeka asilimia 0.4 kutokana na uhitaji mkubwa wa bidhaa hizo kuongezeka ikilinganishwa na miezi 12 iliyopita.

"Kama mnavyofahamu hivi sasa malimao na vitunguu swaumu vinatumika sana, inawezekana mahitaji yameongezeka zaidi na kuchangia kuongezeka kwa bei kuliko ilivyokuwa awali, kwa kipindi cha mwezi mmoja huu," alisema.

Alifafanua kuwa fahirisi hizo zimeongezeka kwa asilimia 0.4 ikilinganishwa na ongezeko asilimia 1.1 lililokuwapo mwezi Februari na Machi, 2020.

"Fahirisi za bei zimeongezeka hadi 120.67 kutoka 120.20 mwezi Machi 2020, kuongezeka kwa fahirisi kumechangiwa na kuongezeka bei kwa baadhi ya bidhaa za vyakula na visivyo vya vyakula, samaki kwa asilimia 1.4, malimao 5.7, vitunguu swaumu 3.4, njegere 4.0, viazi asilimia 4.9 na mihogo asilimia 5.9," alisema.

Alieleza kuwa kwa upande wa bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi Machi na Aprili 2020, ni pamoja na mavazi ya wanawake kama vitenge asilimia 1.5, cherehani asilimia 2.3 na mkaa kwa asilimia 1.6.

# UDSM kuunda mashine za kupumulia

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kimeanza usanifu wa kuunda mashine za kupumulia ya kiotomatiki inayowasaidia wagonjwa waliozidiwa kupumua na kufanya utafiti wa tiba mbadala zinazoonyesha uwezekano wa kuzuia au kupunguza makali ya ugonjwa wa corona.

Hayo yamo kwenye taarifa iliyotolewa jana na Ofisi ya Makamu Mkuu wa Chuo hicho (Utafii), ikielezea mipango mbalimbali ambayo chuo kimejiwekea kusaidia jitihada za serikali kupambana na ugonjwa huo.

Ilisema UDSM pia imejiandaa kutoa fedha za utafiti kuhusu ugonjwa wa corona na imewahimiza watafiti wake kuendelea kufanya utafiti kwa kasi zaidi ili kupata tiba, kinga au njia nyingine ya kudhibiti maambukizo ya ugonjwa wa corona.

"Kupitia Ofisi ya Makamu Mkuu wa Chuo-Utafiti, Chuo kimetenga fedha za utafiti na uvumbuzi kiasi cha Sh. 1,500,000,000 katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 kwa ajili ya mapendekezo yanayohusu athari za maradhi ya Covid-19 na mada nyingine za utafiti," ilisema.

Ilisema UDSM, kupitia Kituo cha Maendeleo na Uhawilishaji wa Teknolojia (TDTC), kimebuni aina mbili za mashine za kunawia mikono za kiotomatiki na zinazotumia miguu.

Taarifa hiyo ilisema mashine hizo zina tangi la lita 250 na zimeandaliwa maalumu kwa ajili ya taasisi zinazohudumia idadi kubwa ya watu kama vile maeneo ya hospitali, viwanda na masoko.

Ilisema mashine hizo zinatoa sabuni ya maji na maji baada ya mtu kusogeza mikono karibu na sensa kwa upande wa mashine za kiotomatiki na kukanyaga pedeli kwa upande wa mashine zinazoendeshwa kwa kutumia miguu.

"Mashine hizi ni nzuri na hazihitaji kufunguliwa kwa mikono hivyo kupunguza uwezekano wa kuambukizana kwa kushika mabomba ya maji, aidha, Chuo tayari kimeshauza mashine hizi katika taasisi kadhaa zikiwamo, Amref, BoT, NHIF, TAA, WFP, TOL, Tamisemi, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Tanesco," ilisema taarifa hiyo.

Ilisema kama mchango wake kwa jamii, UDSM, kupitia TDTC, kinatengeneza mashine 20 za kunawia mikono zitakazotolewa kama msaada kwa hospitali za serikali zilizoandaliwa kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wa Covid-19 jijini Dar es Salaam na mashine zingine zitapelekwa katika vituo vikuu vya mabasi na daladala.

Ilisema kitengo cha vitambaa na nguo cha Idara ya Uhandisi Mitambo na Viwanda kikishirikiana na Kituo cha (TDTC) cha UDSM kimeanza uzalishaji wa barakoa za kiwango cha hali ya juu zenye matabaka matatu.

HABARI KITAIFA

# Bunge laitaka serikali ihifadhi mafuta

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati, imeishauri serikali kutumia vyema mdororo wa bei ya mafuta duniani, ili kupata mafuta kwa masharti nafuu na kuanzisha hifadhi ya mafuta kimkakati kwa ajili ya siku zijazo.

Akiwasilisha maoni ya kamati hiyo bungeni jana, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dunstun Kitandula, alisema ni vyema kwa wakati huu serikali ikazungumza na nchi rafiki zinazozalisha mafuta ili kupata mafuta hayo.

Alisema katika kutekeleza hilo ni vyema Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) liwezeshwe ili kupokea akiba hiyo ya mafuta.

Alisema tayari ulimwengu umeanza kushuhudia Sekta za Usafiri wa Anga na Utalii zikisimama, biashara na uzalishaji viwandani kushuka na hivyo kushuka kwa kiasi kikubwa kwa matumizi ya mafuta na bei yake kuporomoka.

"Kufuatia mkanganyiko huu na mwenendo usiotabirika wa soko la mafuta ulimwenguni, ipo haja kwa nchi yetu kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha nchi inakuwa na akiba ya mafuta ya kutosha wakati wote," alisema.

Kitandula alisema kamati pia ilichambua taarifa kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta nchini na kubaini kuwa, kwa kipindi chote cha Julai 2019 hadi Februari 2020, hali ya upatikanaji wa nishati hiyo ilikuwa nzuri na nchi ilikuwa na akiba ya mafuta ya kutosha kwa wastani wa zaidi ya siku 40 kwa kila aina ya mafuta.

"Hii ni ongezeko la asilimia 55 kulinganishwa na siku 15 za akiba ya mafuta zinazotakiwa kwa mujibu wa kanuni," alibainisha.

Alisema mfumo wa BPS (Bulk procurement System) umewezesha kupungua kwa gharama za meli kusubiri kupakua mafuta kutokana na upangaji na usimamizi mzuri wa uletaji meli za mafuta (laycan) ambao umepelekea muda wa meli kusubiri kupungua kutoka wastani wa siku 45 kwa siku za nyuma hadi wastani wa siku tano kwa sasa.

"Kamati ilibaini kuwa, kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020, gharama za meli kusubiri imepungua kwa asilimia 18.4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/2019,"alifafanua.

Alisema jumla ya lita 4,161,067,814.92 za mafuta ya dizeli, petroli, ndege na taa ziliingizwa kwa matumizi ya ndani ya nchi (local) na nchi za jirani (transit) kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020.

Kitandula ambaye ni Mbunge wa Mkinga, alisema katika kiasi hicho cha mafuta, jumla ya lita 2,398,969,342.12 sawa na asilimia 58 kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, na lita 1,762,098,472.80 sawa na asilimia 42 kwa ajili ya nchi za jirani.

Vilevile, alisema kamati imeridhishwa na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na usimamizi mzuri wa uagizaji wa mafuta unaofanywa na wakala wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (PBPA) kwa kushirikiana na mamlaka nyingine.




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (wa pili kulia), akizungumza baada ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Mwanza, kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba, kumshikilia Mhasibu wa AMCOS ya MHEDI iliyopo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, Paul Nkuba, wafanyabiashara 13 na madalali watatu kwa kosa la kukutwa na mali iliyopatikana kwa njia isiyo halali, kujihusisha na vitendo vya rushwa ya ubadhirifu wa pembejeo za kilimo zenye thamani ya Sh. milion 12.6. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**



## Mbunge CCM kortini makosa 12 uhujumu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Kishapu, Suleiman Nchambi (CCM), jana alipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga na kusomewa mashitaka 12.

Katika kesi hiyo, Upande wa Mashitaka uliongozwa na mawakili watatu wa serikali; Magreth Mdaweka, Jukael Jairo na Nestory Mwenda, ambao walidai mahakamani kwamba mbunge huyo anakabiliwa na makosa 12 ya uhujumi uchumi.

Mshitakiwa anatetewa na Wakili Frank Mwalongo ambaye jana hakupata nafasi ya kuzungumza kortini kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Ushindi Swalo, aliahirisha kesi hiyo hadi itakapotajwa tena Jumatatu ijayo na mshtakiwa alirudishwa mahabusu.

Mei 3, mwaka huu, mbunge huyo alikamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga kwa tuhuma za ujangili na kumiliki silaha kinyume cha taratibu za nchi.

Jeshi hilo lilidai kunasa nyumbani kwa mbunge huyo bunduki 16, risasi 536 na nyama inayodhaniwa kuwa ni ya wanyamapori yenye uzito wa kilogramu 35.

Taarifa ya jeshi hilo kwa vyombo vya habari ilibainisha kuwa mbunge huyo anatuhumiwa kujihusisha na uwindaji haramu katika eneo la Negezi wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.

## Serikali yafafanua kutotangaza wagonjwa wapya wa corona

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema serikali haijatoa taarifa kuhusu mwenendo wa corona nchini kutokana na sababu ya maboresho ya kiufundi kwenye Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii.

Ummy aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kubainisha kuwa mpaka sasa, zipo kazi za kiufundi ambazo zinaendelea.

Alisema ndani ya siku chache, kazi hiyo itakuwa imekamilika na hivyo serikali itaendelea kutoa taarifa kwa umma mara kwa mara kuhusu mwenendo wa ugonjwa huo nchini.

"Wakati hatutoi taarifa za maabara, nitumie fursa hii kuwataka wananchi kuzingatia kuwa ugonjwa wa corona bado upo nchini na ugonjwa huu ni wa hatari na unasambaa kwa haraka. Vilevile, wagonjwa wapo na vifo vinavyotokana na corona vipo.

"Ninawasihi wananchi waendelee kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya na tuondoe hofu, na ni muhimu kutambua kuwa ugonjwa huu tutaendelea kuwa nao kwa miezi kadhaa," alisisitiza.

Waziri huyo alisema wananchi wanapaswa kujifunza kuishi nao huku wakichukua tahadhari ya kujikinga kama yalivyo magonjwa mengine ya kuambukiza.

"Corona ipo, muhimu ni kuondoa hofu na kuchukua tahadhari ya kujikinga dhidi ya ugonjwa huu. "Kwa hiyo, tuendelee na shughuli zetu za ujenzi wa taifa; shughuli za kilimo ziendelee, biashara ziendelee, uvuvi uendelee, uzalishaji mali uendelee, ujenzi uendelee. Kikubwa ni kuchukua tahadhari kila mtu kwa nafasi yake.

"Hili jambo nimeona niliseme kwa sababu tunaweza kujenga hofu kubwa wakati ugonjwa huu utakuwa nao kwa miezi kadhaa.

"Tuchukue tahadhari kwa kunawa mikono kwa sabuni na kwa maji tiririka, kuzingatia umbali usiopungua mita moja kati ya mtu na mtu, ingawa hapa (mkutanoni) sioni kwa waandishi wa habari na mara nyingi huwa ninawaambia," alionya.

RIPOTI MAALUM - 6

# Hasunga: Pesa iko katika shamba la mboga, maua

- Sheria kulinda ardhi ya kilimo yanukia
- Kilimo Kwanza, Kufa Kupona zote ndugu



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akikagua mazao mbalimbali katika banda la maonyesho la Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwenye Viwanja vya Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu Julai 29 mwaka jana. **PICHA: WIZARA YA KILIMO**.

> “Ili uende kulima, unahitaji zana za kisasa, unahitaji dawa. Kwa hiyo, lazima ukatengeneze viwandani, lakini ili navyo viwanda vifanye kazi, vinahitaji malighafi kutoka kwenye kilimo na vinahitaji watu walioshiba.

**Na Sanula Athanas,**

ALIYEKUWA DODOMA

**WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, jana alifichua siri ya Mkoa wa Morogoro kuipiku ‘The Big Four’ (Ruvuma, Mbeya, Iringa na Rukwa) katika uzalishaji wa nafaka nchini na mzizi wa unaommaliza mkulima.**

**Hatua inayofuata katika mwendelezo wa ripoti leo inajikita katika kilimo cha mboga kinavyoweza kuteka tatizo la ajira kwa vijana na mwajiri huyo, bustani na shamba wanavyoandaliwa ulinzi wa kisheria unaotarajiwa kuwasilishwa mapema katika Bunge lijalo. Endelea na ufafanuzi wa wiziri huyo:**

**SWALI: Kilimo Kwanza kipo au hakipo?**

**HASUNGA**: Kilimo kwanza ipo na tangu mimi ninazaliwa nimekuwa ninasikia. Wakati tunapata uhuru, utakumbuka tulikuwa tunasema kilimo cha kufa na kupona. Baba wa Taifa alikuwa anasema ni kufa na kupona.

Baadaye tukaja siasa ni kilimo, tukaja kilimo ni uti wa mgongo, tukaja na kilimo kwanza, sasa hivi tunasema kwamba programu ya Kwa hiyo, ninachotaka niseme ni kwamba kwa kuwa Watanzania walio wengi wanaishi vijijini na wanategemea ajira zao kwenye kilimo, bado kilimo kitaendelaea kuwa ni kilimo kwanza mpaka hapo baadaye sana.

Na ikumbukwe kwamba hakuna nchi yoyote duniani inayoweza kuendelea kiuchumi, ikawa ni nchi ya viwanda bila kuendeleza kwanza sekta ya kilimo.

Kwa hiyo, sisi tunategemea kwamba kilimo ndicho kitakachotoa nafasi ya kuendeleza ujenzi wa viwanda na viwanda vingi vitakuwa ni kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao.

Katika hili, kilimo kitaendelea kuwa ni kilimo kwanza na viwanda vitachukua nafasi ya kuongeza thamani na hivyo ukiviunganisha pamoja, unapata uchumi imara kwa sababu hivyo vinategemeana.

Ili uende kulima, unahitaji zana za kisasa, unahitaji dawa. Kwa hiyo, lazima ukatengeneze viwandani, lakini ili navyo viwanda vifanye kazi, vinahitaji malighafi kutoka kwenye kilimo na vinahitaji watu walioshiba.

Unahitaji watu waliokula vizuri, wenye afya kwenda kufanya kazi kwenye viwanda. Kwa hiyo, hivi vitu viwili vinategemeana na kilimo kitaendelea kuwa ni kilimo kwanza hata kama tutabadilisha majina.

**SWALI: Ni mambo yapi ambayo sasa yanatiliwa mkazo na wizara yako ili sekta ya kilimo iwe na mchango mkubwa zaidi nchini?**

**HASUNGA:** Kwanza, tupo kwenye mkakati wa kubadilisha sera na sheria za kilimo ili tuwe na sheria moja na kuhakikisha kwamba inasimamia kilimo chote.

Lakini pia tunataka tuwe na sheria itakayolinda ardhi ya kilimo. Sasa hivi sehemu zote watu wanabadilisha mashamba na kwenda kupima viwanja.

Sisi tunaona kwamba kama Wizara ya Kilimo kuna shida katika utaratibu ho. Tutahakisha tunatimiza wajibu wetu wa kwanza wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na upatikanaji wa chakula, chakula kinakuwapo ndiyo mambo mengine yanafuata.

Lakini sasa hivi kumekuwa na utaratibu huu niliodokeza wa watu wengi wanabadilisha ardhi ya kilimo, wanaenda kujenga nyumba na viwanda. Lazima ardhi ya kilimo ilindwe kisheria na ndiyo maana tuko kwenye mchakato wa kuandaa muswada wa sheria hiyo.

Jambo la lingine, tunataka sasa hivi twende kwenye kilimo cha kisasa, kilimo cha kibiashara. Sasa hivi ukitoka hapa (Dodoma) mpaka Dar es Salaam, huwezi kuona shamba la mfano, utaona vishamba vidogo vidogo vipo ovyo ovyo. Hili sisi tunahesabu ni kama matumizi mabaya ya ardhi.

Lazima sasa twende kutengeneza vishamba vidogo vidogo, lakini vya mfano kwa kuzingatia ikolojia. Tutalima kwa kuzingatia korosho inastawi zaidi Mtwara na wapi na wapi, kahawa inastawi zaidi wapi, mkonge wapi.

Tunataka tusimamie zaidi ikolojia kwamba mkoa unastawi kitu hiki na hiki na ukitaka kitu fulani, nenda mkoa fulani na tuisimamie. Tunaamini inaweza ikatusaidia kwamba tuwe na uzalishaji unaokwenda kwa mfumo huo.

Jambo lingine tunataka tuwaambie Watanzania, vijana wote ambao wapo nchini wanatafuta ajira. Ni kwenye kilimo tu ambako kumebaki na ajira ambazo hazihitaji utembee na bahasha, utembee na vyeti mtaani unatafuta ajira.

Kwenye kilimo nafasi ziko wazi, ardhi tuliyonayo, bado ni kubwa. Sasa hivi mahitaji ya mbogamboga ni makubwa sana, mahitaji ya matunda ni makubwa sana, mahitaji ya maua duniani ni makubwa.

Kenya wanapata zaidi ya Dola za Marekani bilioni sita kwa mwaka, sisi tunapta chini ya Dola milioni 500 kwa kuuza maua. Tunataka vijana wote tuwahamasishe waende kwenye kilimo cha uhakika, kilimo cha kibiashara.

Vijana wetu wajikite kwenye kilimo cha mbogamboga, kilimo cha matunda, kilimo cha mazao mbalimbali, kila mtu atakavyoweza, lakini tuwawezeshe. Tunaimani uchumi wetu unaweza ukabadilika kwa kiwango kikubwa sana.

# Watoto 2 familia moja wafariki dunia kwa kuangukiwa ukuta

**Na Robinson Wangaso,** MARA

WATOTO wawili Joyce Malima (6) na Christopher Malima (3), wamefariki dunia baada ya kuangukiwa na ukuta wa nyumba walimokuwa wamelala.

Watoto hao walikuwa wamelala na mama yao mzazi Moshi Simon (29), ambaye amejeruhiwa na kulazwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mara.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyakato Mlimali, Malinde Mahamba, alisema tukio hilo lilitokea saa tano usiku Mei 6. Alisema nyumba hiyo ilianguka ukuta upande mmoja na kuwafunika ndipo majirani waliposhtuka baada ya kusikia kishindo na kwenda kuwaokoa na kuwakimbiza hospitali.

Mwenyekiti huyo alisema mtoto mmoja, Joyce alifariki dunia baada ya kufika hospitali na Malima (3), alifariki kabla ya kupatiwa matibabu huku mama yao akilazwa kwa matibabu.

"Ilikuwa muda wa saa tano usiku, huku mvua zikiendelea kunyesha nilipata taarifa kuwa nyumba imeanguka na watu wakiwamo ndani, nilikimbia mpaka eneo la tukio na kukuta mama akiwa ameangukiwa nyumba na watoto wake, tuliomba msaada kwa majirani tulishirikiana na kuwatoa wakiwa hai na kuwakimbiza hospitalini, lakini watoto wote walifariki dunia kabla ya kupata matibabu," alisema.

Alisema nyumba nyingi katika mtaa huo zimejengwa kwa tofali za udongo na kutokana na mvua inayonyesha mkoani hapo inasababisha kuibuka kwa chemchem za maji katika makazi ya watu na nyumba kubomoka.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anano, alitembelea Kata ya Nyakato kukagua hali ya usalama wa wananchi hao na kuwataka viongozi wa serikali za mitaa kuhakiki na kubaini nyumba zilizo katika hatari ya kuangukа ili wanaoishi katika nyumba hizo wahame kuepuka maafa.

Vifo vya watoto hao vimethibitishwa na Kamanda wa Polisi mkoani Mara na miili yao imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani Musoma ikisubiri maziko.



Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Dodoma, Usharika wa Betheli, Mtaa wa Ng'ong'ona, Elineema Mcharo (kulia), akiwa na Katibu wa Kanisa hilo, Emanuel Yesaya, wakiangalia mabaki ya vifaa vilivyokuwa vikitumika kwa ajili ya kubatizia na sakramenti takatifu vilivyoungua baada ya kanisa hilo, kuteketea kwa moto jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wasiojulikana wachoma kanisa KKKT

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATU wasiojulikana wamechoma Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Mtaa wa Ng'ong'ona, Dayosisi ya Dodoma, jijini hapa.

Kwa mujibu wa Askofu wa Kanisa hilo, Amon Kinyunyu, tukio hilo lilitokea juzi jioni.

Kinyunyu alisema watu hao wasiojulikana walichoma kanisa hilo na kuteketeza kila kitu kilichokuwa ndani ikiwamo vifaa vya sakaramenti takatifu.

"Ni kweli jana majira ya saa 11 jioni kanisa letu la Ng'ong'ona lilichomwa moto na watu wasijulikana, lakini hayo yote tunawaachia wenzetu Jeshi la polisi wanalishughulikia kuwabaini wahusika kwa sababu ndio wenye uwezo wa kuwabaini wahalifu hao,"alisema.

Alisema kanisa hilo halikuwa na mgogoro wowote wa eneo hilo na ndio maana hawawezi kujua chanzo cha kuchomwa moto.

Nipashe ilizungumza na baadhi shuhuda wa tukio hilo ambaye pia ni Katibu wa Kanisa hilo, Emanuel Idabu, ambaye alisema mali zingine zilizokuwa ndani ya kanisa hilo ilikuwa ni viti, meza moja, jenereta kubwa na tangi la kuhifadhia maji.

Alisema walipofika eneo hilo wakati moto unawaka hapakuwa na viti hata kimoja jambo ambao linaonyesha wahusika wameiba viti na kuamua kuchoma kanisa ili kupoteza ushahidi.

"Kwa kweli katika hili hatuwezi kusingizia kuwa ni mgogoro wa kidini, hapana hawa ni watu wenye nia mbaya baada ya kuiba viti wakaona wateketeze kanisa letu ili kupoteza ushahidi," alisema.

Mchungaji wa kanisa hilo, Elineema Mcharo, alisema lilijengwa mwaka jana na lilikuwa bado halijaunganishwa umeme.

Hata hivyo alisema baraza la wazee wa kanisa hilo litakaa ili kuona namna ya kuendelea kutoa huduma kwa waumini wa mtaa huo.

Nipashe ilipomtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto alikikiri kuwapo kwa tukio hilo na kwamba ametuma askari wake kwenda eneo la tukio na kuahidi kutoa ufafanuzi.

# Hospitali Kisarawe kutengeneza vazi corona

**Na Maulid Mmbaga**

KATIKA jitihada za kupambana na ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona, Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, imefanikiwa kutengeneza mavazi ya kujikinga na marazi hayo (PPE).

Hayo yameelezwa jana na Mkuu wa Wilaya wa Kisarawe, Jokate Mwegelo, kupitia ukurasa wake wa instagram kuwa hospitali hiyo imefikia hatua hiyo ikiwa ni jitihada za kuwakinga wauguzi wake dhidi ya maambukizo ya corona.

Alisema, pia kwa kushirikiana na hospitali hiyo walianza kutengeneza barakoa na vitakasa mikono ambavyo tayari vimekamilika na vinapatikana katika duka la dawa la wilayani hapo.

"Kuhusiana na ubora wa vazi letu la PPE, quality (ubora) ni kama ile ya Muhimbili kwa maana ya material iliyotumika lakini pia kwa maana ya uimara yetu imeongezwa uimara wa ndani kuzuia isichanike/kutatuka haraka wakati wa kuitumia," alisema.

Alipongeza timu ya dharura ya hospitali hiyo kwa hatua hiyo kwa kuwa itasaidia kuwakinga madaktari na kuwafanya watimize majukumu yao kwa ufanisi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kanuni mpya Ligi Kuu Bara zisisahau majanga

**WAKATI** hatima ya Ligi Kuu Tanzania Bara bado ikiwa haijajulikana kutokana na kuwapo kwa maambukizo ya ugonjwa wa corona, tayari msimu wa 2019/20 wa ligi hiyo ulikuwa unaelekea ukingoni.

Mbali na Ligi Kuu Tanzania Bara, pia Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili, Ligi Kuu ya Wanawake na mashindano ya Kombe la FA, yaliguswa na agizo la serikali la kuzuia mikusanyiko.

Kumalizika kwa msimu huu, maana yake ni kuanza kwa maandalizi ya msimu mpya wa 2020/21.

Kuna kauli inayosemwa kuwa, unaweza kupotea wakati wa kwenda, lakini kamwe huwezi kupotea wakati wa kurudi.

Nipashe limekumbusha kauli hii kwa maana ya kuwataka wadau wote wa soka nchini, wakiongozwa na wasimamizi, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuhakikisha wanaboresha kanuni zake.

Kipengele ambacho leo hii Nipashe inakikumbusha ni kuweka kanuni inayoelekeza uamuzi utakaochukuliwa endapo kutatokea janga la aina yoyote ambalo litasababisha ligi hizo kushindwa kuendelea.

Leo hii TFF imekuwa na kigugumizi kuhusiana na kumaliza kwa msimu huu, kwa sababu kanuni zake zilikuwa hazielezi lolote endapo janga la corona litatokea. Hii imesababisha shirikisho hilo pamoja na viongozi wa serikali kufanya vikao mbalimbali kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa suala hili.

Kama vile imejidhihrisha kuwa kanuni zake zilikuwa na upungufu, kwa kushindwa kuweka tahadhari, TFF imeshindwa kutangaza kama baadhi ya mataifa yalivyofanya kwa kuhofia lawama kutoka kwa klabu ambazo zitaathirika na uamuzi hasa wa kuutambua msimamo uliopo.

Kwa upande wa timu inayoongoza kwenye msimamo inaweza kufurahia kwa kutangaza mabingwa wapya hali ya kuwa hawakumaliza mechi, lakini timu zinazofuata zitalalamika kwa sababu huenda wangefanya vizuri katika michezo iliyobakia na hatimaye kuwaondoa kileleni waliokuwa wanaamini tayari wamemaliza kazi.

Pia kwa klabu ambazo zilikuwa zinaburuza mkia pia zingeona hazijatendewa haki ya kushushwa daraja kwa sababu huenda zingefanya 'maajabu' katika michezo yake iliyobakia na hatimaye kujinasua na janga la kushuka daraja.


Nipashe tunawakumbusha TFF na wanachama wake ambao ni vilabu, kuweka kanuni ambayo itasaidia kutoa uamuzi utakaopokelewa na timu zote bila ya kuwapo kwa malalamiko yoyote na maandalizi ya msimu mpya yakaruhusiwa kuanza.

Lazima tujifunze majanga ni sehemu ya maisha ya mwanadamu na kwa kutambua hilo, kanuni za msimu ujao ziangalie suala hili kama ambavyo ilikubaliana pale mechi zinapovunjika kwa sababu ya janga la mvua au sababu nyingine ya kiusalama iliyoelezwa katika kanuni hizo.

Kilichotokea msimu huu, kiwe fundisho kwa viongozi wetu wa soka nchini na michezo mingine kujiandaa kukabiliana na changamoto mbalimbali na hatimaye kuruhusu maisha mengine yaendelee.

Hakuna jambo lisilokuwa na suluhisho, endapo viongozi wetu watalijadili kwa 'uzito' na kuacha kuchagua vipengele vya kuboreshwa kwenye kanuni za ligi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Barnabas Maro

# Mwisho wa malalamiko ya Ligi Kuu?

**ENDAPO** kusudio la Rais John Pombe Magufuli litatekelezwa baada ya mawasiliano ya hapa na pale, bila shaka timu 19 za Ligi Kuu ya msimu huu wenye utata wa corona, zitafurahia isipokuwa moja ndio itakayosononeka kwa kucheleweshewa kombe lao.

Hiyo ni timu ya Simba, maarufu 'Wekundu wa Msimbazi.' Sipendi kuiita 'mnyama' kama walivyozoea waandishi wa michezo, kwani 'mnyama' ni hayawani yaani mnyama wa miguu minne ilhali wachezaji wa Simba ni binadamu kama wengine wenye miguu miwili.

Napata ukakasi wa kutumia jina hilo kwa wachezaji wa klabu ya Simba kwani maana nyingine ya mnyama ni tamko la kumtusi mtu. Nasisitiza kuwa ni 'watani wetu wa jadi' kwa maneno lakini si kwa vitendo. Watani hawadhuriani bali husaidiana kwa kila hali lakini si kwa Simba na Yanga! Kila moja inaiombea nyingine mabaya. Huo si 'utani wa jadi' bali ni 'chuki za jadi!'

Mpaka Ligi Kuu ilipositsimamishwa kutokana na ugonjwa mpya unaoitwa corona ukiendelea kuitikisa dunia, bingwa mtetezi, Simba ilikuwa ikiongoza kwa alama 71 baada ya kucheza mechi 28 ikifuatiwa na Azam FC pia iliyocheza mechi 28 lakini ikiwa na alama 54 na Yanga ikiwa nafasi ya tatu kutoka juu imecheza mechi 27 na kuambulia alama 51.

Tukirudi chini, timu ya mwisho inayolemewa kwa uzito wa kuzibeba timu 19 zilizo juu yake, ni Singida United yenye alama 15 baada ya michezo 29 ikiwa na mabao 16 ya kufunga na kufungwa 49. Ni timu pekee iliyofungwa mabao mengi zaidi ya zingine. Juu ya kichwa chake ni timu ya Mbao yenye alama 22 kwa kukubali kufungwa mabao 33.

Kwa mwenendo huo huo wa kwenda juu, kuna timu ya Alliance FC yenye alama 29 na kufungwa mabao 36 ilhali Mbeya City ikiwa kichwani mwa Alliance kwa alama 30 na kuambulia mabao 35 ya kufunga. Timu zote hizi zipo hatarini kushushwa daraja endapo hazitapanda juu kama ligi ikiendelea.

Ikumbukwe pia kwamba wakati mwingine kandanda ni mchezo unaoshangaza kwani umdhaniaye siye aweza kuwa ndiye na adhaniwaye ndiye akawa siye!

Katika hali hii, kila timu itacheza kwa bidii ili zile zinazoifuatia Simba, yaani Azam, Yanga, Namungo na Coastal Union zisishuke chini ya hapo zilipo bali zisalie kwenye nafasi za juu katika msimamo wa ligi hiyo.

Wakati hali ikiwa hivyo, kuna manung'uniko ya chini kwa chini yanayotolewa na wapenzi, mashabiki na hata viongozi wa Simba wakitaka wakabidhiwe kombe kwani hata ligi ikiendelea haiwezi kukosa kombe iwe jua iwe mvua. Maana yake ni kwamba hakuna timu itakayofikia idadi ya alama ilizo nazo.

Ni kweli kwamba timu zilizo chini ya Simba hakuna itakayoweza kuipiku kwani ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya zingine. Husemwa kandanda ni mchezo wa bahati. Sawa, lakini mpaka Ligi ilipositsimamishwa, Simba ilikuwa na alama nyingi (71) zaidi na mabao 63 ikifungwa mabao 15. Pia imetoka sare mara mbili na kupoteza michezo mitatu.

Wakati Azam FC iliyo nafasi ya pili ikiwa na mabao 37 ya kufunga na kufungwa 20, imecheza michezo 28 kama Simba lakini meshinda michezo 16 na kupoteza 6. Yanga nayo imecheza michezo 27, imeshinda 14, imetoka sare mara 9, kufungwa mara 4 ikiwa na mabao 31 na kufungwa 20.


Namungo imecheza mechi 28 ikishinda mechi 14 kama Yanga, sare mara 8 na kupoteza michezo 6, mabao 34 ya kufunga na kufungwa mabao 25. Coastal Union ambayo ipo kwenye hatari ya kumpoteza mchezaji wao Bakari Mwamnyeto kusajiliwa na Azam, Simba au Yanga msimu ujao imecheza mechi 28, imeshinda mara 13, imepata sare 7 na kupoteza mechi 8 na kupata mabao 27, dhidi ya mabao 19 waliyofungwa na kupata alama 46. Husemwa kandanda ni mchezo usiotabirika lakini kwa hali yoyote itakavyokuwa kwa Ligi ya mwaka huu, itakuwa ni ajabu Simba kupoteza mechi nyingi zitakazoifanya ipokonywe kombe ililotwaa mara mbili mfululizo misimu miwili iliyopita hata ishindwe kulitwaa moja kwa moja mwaka huu.

Kama Ligi itasimamishwa na Simba kupewa ushindi, italeta shida kwa timu zinazowania nafasi za pili, tatu na nne na mbaya zaidi timu zitakazojitahidi kuepuka kushuka daraja kwa sababu nazo zitalalamika kwa kutopewa nafasi ya kukwepa kadhia hiyo.

Kwa maana hiyo, viongozi wa Simba wanapaswa kuwa waungwana kwa kukubali Ligi Kuu iendelee badala ya kukabidhiwa kombe ilhali ligi hiyo haijamalizika. Sisemi wachezaji wa Simba waingie uwanjani kwa dharau, La hasha. Wanatakiwa kudhihirisha ubingwa wao wa mara ya tatu mfululizo, vinginevyo watapoteza heshima yao kama watacheza kwa dharau na kusababisha wakose kombe!

marobarnabas@yahoo.com 0784 334 096

TANGAZO


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHESHIMIWA DKT. HAMISI KIGWANGALLA (MB) WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021
MHE. DKT. HAMISI KIGWANGALLA (MB), WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII
PROF. ADOLF MKENDA KATIBU MKUU
MHE. CONSTANTINE KANYASU NAIBU WAZIRI
DKT. ALOYCE NZUKI NAIBU KATIBU MKUU

# HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII

## MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHESHIMIWA DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA (MB) WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,***kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

2. ***Mheshimiwa Spika,***awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwatumikia Watanzania. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Nachukue fursa hii kumshukurukwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo ameongoza nchi yetu kwa busara na ujasiri wa hali ya juu na kwa mamna ambavyo uongozi wake umeiwezesha Wizara ya Maliasili na Utalii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Natoa pia shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu; kwa kuniongoza katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Wizara kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na miongozo mingine. Kupitia uongozi wa Mheshimiwa Rais na viongozi wengine wakuu, Wizara imeendelea kutimiza wajibu wake kwa kuimarisha uhifadhi na kuendeleza utalii kwa ufanisi zaidi na hivyo kuchangia katika juhudi za kukuza uchumi na ustawi wa wananchi.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** ninakupongeza wewe binafsi pamoja na Uongozi wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi. Aidha, ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota, Mbunge, ambayo pamoja na mambo mengine, imejadili, kushauri kutoa maoni na kupitisha Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Wizara itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaungana na waheshimiwa wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge, kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na mazingira; na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge,kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki.

5. ***Mheshimiwa Spika,***kwa masikitiko makubwa ninaungana na Waheshimiwa Wabunge kutoa salamu za pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu, wananchi na familia za marehemu kwa kuondokewa na Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini; Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve; na Mheshimiwa Dkt. Augustino Philip Mahiga, Mbunge na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, Amina.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Mheshimiwa Constantine J. Kanyasu (Mb), Naibu Waziri; Profesa Adolf F. Mkenda, Katibu Mkuu; na Dkt. Aloyce K. Nzuki, Naibu Katibu Mkuu; wakurugenzi na wakuu wa vitengo; wakuu wa mashirika na taasisi zilizo chini ya Wizara; watumishi na wadau wote kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara na hatimaye kuweza kuwatumikia wananchi kwa ufanisi zaidi.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Nzega Vijijini kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninamshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Dkt. Bayoum Kigwangalla na familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na dua katika utekelezaji wa majukumu yangu.

### B. MCHANGO WA MALIASILI NA UTALII KATIKA UENDELEZAJI WA UCHUMI WA VIWANDA

8. ***Mheshimiwa Spika,***maliasili na utalii ni miongoni mwa sekta za uchumi nchini ambazo zinatoa mchango mkubwa katika ukusanyaji wa mapato na kuendeleza maisha ya Watanzania wengi ikiwepo fursa za kutoa ajira. Mathalan, Sekta Ndogo ya Utalii kupitia vivutio mbalimbali inachangia zaidi ya asilimia 17 ya pato la Taifa, asilimia 25 ya fedha zote za kigeni na kuajiri zaidi ya watu milioni 5.5 kwa mwaka. Kutokana na umuhimu huo, Wizara inatoa rai kwa wadau wote kwa ujumla kuendelea kushirikiana na Wizara katika kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinaendelea kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu.

**Athari za Ugonjwa wa Corona (COVID-19) katika Sekta ya Utalii**

9. ***Mheshimiwa Spika,*** utalii duniani na hapa nchini umeathirika kutokana na mlipuko wa homa kali ya mapafu ujulikanao kama *COVID-19*. Katika kukabiliana na janga hili, mataifa ambayo ni masoko muhimu ya utalii nchini katika mabara ya Ulaya, Amerika Asia na kwingineko duniani, yamechukua hatua mbalimbali za kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huu. Hatua hizo zinajumuisha kuzuia raia wake kusafiri. Kwa sababu hiyo mashirika ya ndege takriban yote yamesitisha kufanya safari za kimataifa za abiria. Hali hii imeleta anguko kubwa katika sekta ya utalii hapa nchini na duniani kote. Hali hii itachukua muda kurejea katika hali ya kawaida. Hata janga hili la COVID-19 likiisha bado utalii utaendelea kuathirika hapa nchini kwa muda mrefu kutokana na mdororo wa uchumi duniani ambao unatokana na mtikiso wa janga hili. Hata kama tukijipa matumaini makubwa kabisa, ambayo kwa kweli ni matumaini tu, kwamba janga hili litaisha Mwezi Oktoba na kwamba hakutakuwa na athari za mdororo wa uchumi baada ya hapo, bado madhara kwenye sekta ya utalii yatakuwa ni makubwa sana kama ifuatavyo; idadi ya ajira za moja kwa moja katika Sekta ya Utalii zitashuka kutoka **622,000** zilizotarajiwa hadi kufikia 146,000; idadi ya watalii itashuka kutoka 1,867,000 waliotarajiwa hadi kufikia watalii 437,000. Katika hali hiyo mapato ya Serikali kutoka katika Sekta ya Utalii yatashuka kutoka Shilingi trilioni **2.7** zilizotarajiwa hadi kufikia Shilingi **bilioni 598.** Kwa vyovyote, hali inaweza kuwa ngumu zaidi kuliko maoteo haya ya matumaini yanavyoonesha.

10. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara ya Maliasili na Utalii imefanya uchambuzi na tathmini ya athari za COVID-19 kwenye sekta nzima ya utalii. Taarifa ya uchambuzi na tathmini hii pamoja na mapendekezo kadhaa, ambayo ilihusisha wadau na wataam kadhaa, ilishawasilishwa HAZINA ili iunganishwe na uchambuzi mpana na tathmini ya kina ya athari za janga ili kwenye uchumi wa nchi yetu. Mapendekezo ya Taarifa hii ambayo yako chini ya mamlaka ya Wizara tayari yamefanyiwa kazi.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** madhara haya ya COVID-19 yameathiri sana taasisi zetu ambazo kwa kawaida zinachangia sana kwenye uchumi wanchi yetu. Kwa mfano, katika mwaka 2020/2021 TANAPA ililenga kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 363.9, lakini kutokana na hali inavyoendelea makisio sasa yanakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 64; NCAA ilikadiria Shilingi bilioni 162.7, sasa ni Shilingi bilioni 58; TFS ilikadiria Shilingi bilioni 153.6, sasa ni Shilingi bilioni 121; na TAWA ilikadiria Shilingi bilioni 58.1, sasa ni Shilingi bilioni 22. Kwa takwimu hizi, mapato yanatarajiwa kushuka kwa takriban asilimia 75. Upungufu huo wa mapato ni mkubwa kwa sekta na unaweza kusababisha baadhi ya taasisi za uhifadhi zilizo chini ya Wizara kushindwa kujiendesha. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara imeendelea kuwashirikisha wadau wa sekta ili kuweka mikakati ya namna ya kuisaidia sekta isiathirike zaidi.

### C. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

***Ukusanyaji Maduhuli***

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi bilioni 71.54** kutoka vyanzo vya idara, mifuko na taasisi. Hadi Machi 2020, **Shilingi bilioni 47.01** zimekusanywa sawa na asilimia 66 ya makadirio. Aidha, mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFS yaliidhinishiwa kukusanya **Shilingi bilioni 701.81**. Hadi Machi 2020, mashirika hayo yalikuwa yamekusanya **Shilingi bilioni 503.87** sawa na asilimia 72 ya makadirio. Hata hivyo, ukusanyaji wa mapato unaendelea kukabiliwa na changamoto ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 ambao utaathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFS. Mathalan kwa kipindi cha robo ya nne, taasisi hizo zilikadiria kukusanya **Shilingi bilioni 132.18** lakini kutokana na athari za mlipuko huo, taasisi hizo zinatarajia kukusanya **Shilingi bilioni 33.46** sawa na anguko la asilimia 75.

***Matumizi ya Kawaida na Maendeleo***

13. ***Mheshimiwa Spika,***katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara iliidhinishiwa kutumia **Shilingi bilioni 120.20** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi bilioni 71.31** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 48.89** ni miradi ya maendeleo. Hadi Machi 2020, Wizara ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 61.45** sawa na asilimia 51 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 47.66** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 13.79** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mafanikio ya Wizara kwa mwaka 2019/2020**

14. ***Mheshimiwa Spika,***katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo:-

***Udhibiti wa Ujangili na Uvamizi wa Maeneo ya Hifadhi***

15. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara imeendelea kuongeza ufanisi katika kukabiliana na ujangili, biashara haramu ya nyara, mazao ya misitu na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Taarifa za ufuatiliaji wa matukio hayo zinaonesha kuwa ujangili umepungua kwa takriban asilimia 80. Aidha, uvunaji haramu wa miti iliyo hatarini kutoweka na uvamizi katika misitu ya hifadhi umepungua

# HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII

kwa takribani asilimia 85. Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa ulinzi ambapo jumla ya siku - doria 402,208 zimefanyika na kuwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 9,085 waliochukuliwa hatua mbalimbali za kisheria.

*Kuongezeka kwa Mapato yatokanayo na Utalii*

16. ***Mheshimiwa Spika,***mapato yatokanayo na utalii wa kimataifa yameongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.4 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Bilioni 2.6 mwaka 2019. Aidha, wastani wa siku za kukaa watalii nchini zimeongezeka kutoka siku 10 mwaka 2018 hadi siku 13 kwa mwaka 2019. Vilevile, matumizi ya watalii kwa siku yameongezeka kutoka Dola za Marekani 193 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani 266 mwaka 2019. Mafanikio hayo yametokana, pamoja na mambo mengine jitihada za kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi.

*Kupandishwa Hadhi Maeneo ya Hifadhi*

17. ***Mheshimiwa Spika,***Serikali imeongeza idadi ya Hifadhi za Taifa kutoka 16 hadi 22 na misitu ya hifadhi ya mazingira asilia kutoka 17 hadi 19. Ongezeko la Hifadhi za Taifa limetokana na kupandisha hadhi mapori ya akiba ya Burigi, Biharamulo, Kimisi; Ibanda; na Rumanyika - Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa za Burigi - Chato, Ibanda - Kyerwa na Rumanyika - Karagwe; sehemu ya Pori la Akiba Selous kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere; sehemu ya Pori la Akiba Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla na Pori la Akiba Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi. Aidha, ongezeko la misitu ya hifadhi ya mazingira asilia limetokana na kupandisha hadhi misitu ya hifadhi ya Uzigua na kuunganishwa kwa misitu mitatu ya Pugu, Kazimzumbwi na Vikindu kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Pugu- Kazimzumbwi.

*Mapitio ya Kanuni na Miongozo Mbalimbali*

18. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara imeandaa Kanuni za Uuzaji wa Nyamapori, Kanuni za Uwekezaji wa Miundombinu ya Utalii katika Misitu ya Hifadhi na Kanuni za Uwekezaji katika Maeneo Maalumu ya Wanyamapori. Aidha, Wizara imepitia Kanuni za Huduma za Malazi zamwaka 2015 na Kanuni za Ufugaji wa Wanyamapori za mwaka 2013. Kanuni hizi zitasaidia katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya maliasili na utalii.

*Kuendeleza Mashamba na Upandaji Miti*

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TFS imepanda jumla ya hekta 8,726 za miti kwenye mashamba 23 ya Serikali Kuu. Aidha, jumla ya miche ya miti milioni 7.6 imegawiwa na kupandwa na wananchi ikijumuisha miche 800,000 iliyopandwa katika Jiji la Dodoma kupitia Kampeni ya Dodoma ya Kijani.

*Kukamilisha Taratibu za Mfumo wa Jeshi Usu*

20. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara imetoa mafunzo ya utayari kwa watumishi 4,556 kutoka taasisi za TANAPA, NCAA, TAWA na TFS ikiwa ni maandalizi ya utekelezaji wa mfumo wa Jeshi Usu. Aidha, Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali unaojumuisha Sheria za Wanyamapori Sura 283, Sheria ya Misitu Sura 323, Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro Sura 284 kuhusu kuanzishwa rasmi kwa Jeshi hilo umeandaliwa na kusomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge la 11, Mkutano wa 18 tarehe 28 Januari, 2020.

*Uendelezaji wa Maeneo ya Malikale*

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha ukarabati wa Nyumba ya Makumbusho ya Dkt. David Livingstone, Kigoma - Ujiji na miundombinu ya barabara yenye urefu wa kilometa tano katika Kituo cha Michoro ya Miambani Kolo, Kondoa. Aidha, ukarabati wa Makumbusho ya Nyumba ya Utamaduni na majengo ya Kijiji cha Makumbusho katika Mkoa wa Dar esSalaam pamoja na Makumbusho ya Azimio la Arusha umekamilika.

**Utekelezaji wa Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Wanyamapori**

*Ulinzi wa Wananchi Dhidi ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu*

22. ***Mheshimiwa Spika,***katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imetengeneza mfumo unaoruhusu wananchi kutoa taarifa za matukio kupitia simu za mkononi kwenye namba maalum iliyotolewa na Wizara. Aidha, Wizara imeendelea kutumia teknolojia ya kuwafunga baadhi ya ndovu vifaa maalum vya kielekitroniki kwa lengo la kufuatilia nyendo zao ili kuepusha migongano na wananchi wanaoishi kando ya maeneo yaliyohifadhiwa.

23. ***Mheshimiwa Spika,***hadi Februari, 2020 Wizara imelipa jumla ya Shilingi 984,768,000 kwa waathirika 9,060 kama kifuta machozi na kifuta jasho. Aidha, Wizara kupitia TAWAimefanya jumla ya siku doria 6,612za kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu ambapo wanyamapori wakali 61waliuawa baada ya kuhatarisha maisha ya wananchi na mali zao. Vilevile, Wizara imehamisha jumla ya simba 36 waliokuwa wanahatarisha maisha ya watu na mifugo kutoka Wilaya ya Serengeti na makundi sita (6) yenye mbwa - mwitu 83 katika Wilaya ya Loliondo na kuwapeleka katika maeneo ambayo hawataleta madhara.

*Kuimarika na Kuongezeka kwa Umaarufu wa Tanzania katika Uhifadhi*

24. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara imeendelea na juhudi za kuimarisha uhifadhi, usimamizi na utangazaji wa vivutio vya utalii. Kupitia jitihada hizo, Hifadhi ya Taifa Serengeti kupitia uratibu wa Kampuni ya *World Travel Awards* imetangazwa kuwa hifadhi bora katika Bara la Afrika na kupata tuzo. Pamoja na mambo mengine, umaarufu huo umetokana na kuwepo kwa uhifadhi endelevu wa wanyamapori watano muhimu yaani simba, ndovu, nyati, chui na faru pamoja na wingi wa nyumbu na matukio yake ya kuhama kati ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na Hifadhi ya Maasai Mara ya nchini Kenya.

*Uwindaji wa Kitalii*

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utaratibu wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada wa kielekitroniki ambao umeongeza uwazi, uwajibikaji na kuruhusu nguvu ya soko kuamua bei ya vitalu. Awamu ya kwanza ya mnada ilifanyika Juni, 2019 ambapo jumla ya vitalu sabakati ya 26 vilivyotangazwa viliuzwa na kuingiza jumla ya Dola za Marekani 831,000 sawa na asilimia 98 ya ada ya vitalu vyote 26 endapo utaratibu wa zamani ungeendelea kutumika.

**Utekelezaji wa Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki**

*Ufugaji Nyuki na Masoko ya Mazao ya Nyuki*

26. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara kupitia mfuko wa Misitu wa Tanzania imetoa mafunzo ya ufugaji nyuki kwa wananchi 1,225 na vikundi 144; mizinga 5,288 na seti 160 za mavazi ya ufugaji nyuki. Aidha, Mfuko umewezesha ujenzi wa viwanda vipya viwili katika mikoa ya Tabora (Sikonge) na Geita (Bukombe); na kuanza kwa ukarabati wa viwanda vitatu katika mikoa ya Katavi (Mlele), Kigoma (Kibondo) na Singida (Manyoni). Vilevile, Wizara kupitia Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora imeanzisha mradi na mafunzo maalum ya kuzalisha malkia.

*Udhibiti wa Moto*

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TFS imeendesha jumla ya mikutano 229 kwenye vijiji 239 katika wilaya 35, kujenga minara minne ya kufuatilia matukio ya moto na kukarabati minara 19. Aidha, Wizara imenunua mtambo maalum wa kuzima moto wa msituni wenye uwezo wa kuzima moto hadi umbali wa mita 100. Vilevile, mipaka yenye urefu wakilometa 81,223 imesafishwa katika misitu 89. Kutokana na jitihada hizo, matukio ya moto yamepungua kutoka asilimia 11 mwaka 2018 hadi asilimia nane mwaka 2019.

**Utekelezaji wa Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Utalii**

*Kuendeleza Mazao ya Utalii*

28. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara imeandaa mkakati wenye matokeo ya haraka wa uendelezaji wa mazao ya utalii wa fukwe, meli na utalii wa mikuatano. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Songwe na Morogoro Septemba, 2019 ilifanya Jukwaa la Uwekezaji katika Sekta ya Utalii. Pia, Onesho la Utalii Karibu Kusini lilifanyika sanjari na Jukwaa hilo kwa lengo la kufungua fursa za utalii na uwekezaji katika Ukanda wa Kusini. Aidha, Machi 2020, Wizara kwa kushirikiana na mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kigoma na Tabora ilizindua maandalizi ya Onesho la Kimataifa na Jukwaa la Uwekezaji lijulikanalo kama *Great Lakes International Tourism Expo (GLITE)*ambalo kama isingekuwa kuzuka kwa janga la virusi vya Corona lingefanyika mwezi Juni, 2020.

**Kutangaza Utalii wa Ndani**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** utalii wa ndani ni muhimu kwa sababu tatu kuu. Kwanza, unatoa fursa ya wananchi kupumzika kwa namna nzuri zaidi. Pili, unasaidia kufanya wananchi wathamini zaidi vivutio tulivyonavyo na hivyo kuongeza mwamko wa kuhifadhi na kuvitunza. Tatu, ni chanzo cha mapato kwa taasisi zetu za uhifadhi, jambo ambalo ni muhimu sana hususan kwa sasa ambapo watalii kutoka nje wameshindwa kuja kwa sababu ya janga la Ugonjwa wa Corona.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha utalii wa ndani nchini, Serikali imeanzisha chaneli maalum iitwayo Safari Channel kwenye Shirika la Utangazaji la Taifa. Chaneli hii imesaidia sana kuonesha vivutio mbalimbali tulivyonavyo hapa nchini ili kuhamasisha Watanzania kuvitembelea. Wadau mbalimbali pia wameunga mkono juhudi za kukuza utalii wa ndani kwa kuandaa na kushiriki katika matukio mbalimbali kama vile Twendezetu Burigi, HK Kilimanjaro Challenge, Mkwawa Trails Run, Rock City Marathon, Ngorongoro Marathon, Kigamboni Marathon, Selous Marathon, Morogoro Marathon na Serengeti Marathon. Aidha, pamoja namatukio hayo, Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali za kuutangazia umma wa Watanzania kuhusu vivutio vyetu kwa njia mbali mbali, zikiwemo kuadhimisha miaka 60 ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kuendelea kuhamasisha matumizi ya utambulisho wa Taifa letu (*Tanzania Unforgettable*) katika kukuza zaidi utalii nchini. Kupitia jitihada hizo, takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka 2019, jumla ya wafuatiliaji (followers) 1,064,215 walisambaza ujumbe kupitia mitandao ya kijamii (facebook, twitter, instagram, youtube na destination portal user) na kushawishi Watanzania kutembelea vivutio vya utalii. Takwimu hizo zikilinganishwa na mwaka 2018, kuna ongezeko la wafuatiliaji 286,900 sawa na asilimia 37.

**Miradi ya Maendeleo**

31. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara imeendelea kutekeleza miradi 11 ya maendeleo ambayo inalenga Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini; Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili; Usimamizi Endelevu wa Maliasili; Kuendeleza Misitu ya Hifadhi ya

# HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII

Mazingira Asilia; Kujenga Uwezo wa Taasisi za Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki; Kujenga Uwezo wa Jamii katika Kusimamia Misitu kwa Tija na Misingi Endelevu; na Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu.

32. ***Mheshimiwa Spika,***maelezo ya kina juu ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/2020 yamefafanuliwa **kuanzia Aya 24 hadi 113 ya Kitabu cha Hotuba**.

## D. CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

***Changamoto***

33. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ni pamoja na: kuwepo uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na maeneo ya shoroba; kuongezeka kwa migongano kati ya binadamu na wanyamapori; uhaba wa watumishi pamoja na wafanyakazi wenye ujuzi na utaalamu katika fani mbalimbali, hususan katika fani ya ukarimu; kuharibika kwa miundombinu ya barabara kutokana na mvua nyingi zilizonyesha; pamoja na mlipuko wa ugonjwa wa Corona (COVID-19) duniani.

***Utatuzi wa Changamoto***

34. ***Mheshimiwa Spika,***katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali na kushirikisha wadau katika kuhifadhi maliasili na malikale na kuboresha miundombinu katika maeneo yaliyohifadhiwa na vivutio vyautalii. Aidha, Wizara imeimarisha ulinzi kwa wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu, kuhamasisha na kutekeleza mikakati ya upandaji miti, kuanzisha na kuendeleza viwanda vya mazao ya misitu na nyuki, kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili na malikale. Vilevile, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau katika kuendeleza na kuimarisha vyuo vya mafunzo ya utalii na kutumia njia za kielekitroniki kuwafahamisha kuhusu vivutio mbalimbali vya utalii na kuwahamasisha kuvitembelea baada ya ugonjwa wa Corona kudhibitiwa.

## E. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

35. ***Mheshimiwa Spika,***katika mwaka 2020/2021, Wizara itajikita katika kusimamia na kuendeleza sekta zake ili ziweze kuendelea kuchangia ipasavyo katika uchumi wa Taifa letu. Maeneo ya mpango huo ni pamoja na:-

***Ukusanyaji Maduhuli***

36. ***Mheshimiwa Spika,***kwa mwaka 2020/2021, Wizara inakadiria kukusanya **Shilingi bilioni 65.26** kutoka katika vyanzo vya idara, mifuko na taasisi zilizo chini yake. Kati ya fedha hizo, idara zitakusanya**Shilingi bilioni 22.66**; taasisi zinazopata ruzuku zitakusanya **Shilingi bilioni 18.85**; na Mifuko ya uhifadhi ya TWPF na TaFF itakusanya **Shilingi bilioni 23.75.**Aidha,Mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFS yanakadiria kukusanya **Shilingi bilioni 738.23.** Kati ya fedha hizo,TANAPA itakusanya **Shilingi bilioni 363.91,** NCAA **Shilingi bilioni 162.66,**TAWA **Shilingi bilioni 58.06** na TFS **Shilingi bilioni 153.60.**

***Matumizi ya Kawaida na Maendeleo***

37. ***Mheshimiwa Spika,***kwa mwaka 2020/2021, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi bilioni 114.59.** Kati yafedha hizo, **Shilingi bilioni 69.57** nikwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 45.02** nimiradi ya maendeleo. Makadirio ya matumizi ya kawaida yanajumuisha mishahara **Shilingi bilioni 50.85** na matumizi mengineyo **Shilingi bilioni 18.72.**Aidha, **Shilingi bilioni 45.02** zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo.Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 44.32** zitatoka kwa washirika wa maendeleo na **Shilingi milioni 700** zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali**.**

**Kazi zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake kwa 2020/2021**

***Sekta Ndogo ya Wanyamapori***

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia sekta ndogo ya wanyamapori itaendelea kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori, kukamilisha mapitio ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, Sheria ya TANAPA, NCAA na TAWIRI; na kuandaa Sheria ya kuanzisha TAWA. Aidha, Wizara itaratibu upandishaji hadhi mapori tengefu ya Inyonga, mbuga ya Wembere na misitu ya Litumbandyosi - Gesimazowa kuwa mapori ya akiba na kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) Kilosa Moani. Vilevile, Wizara kupitia TANAPA itaimarisha ulinzi na usimamizi wa hifadhi za Taifa; na kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali katika hifadhi ili kuwezesha shughuli za utalii kufanyika.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia NCAA itaendelea kuboresha miundombinu kwa kukarabati barabara, viwanja vya ndege ndani ya eneo la hifadhi; na kukamilisha mapitio ya matumizi mseto ya ardhi, sheria iliyoanzisha Mamlaka na Mpango wa Jumla wa Matumizi ya Eneo. Aidha, kupitia TAWA, Wizara itafanya siku doria 337,517katika mapori ya akiba, mapori tengefu, maeneo ya ardhioevu na WMAs; na kuimarisha ulinzi wa wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, TAWIRI itaidadi wanyamapori nchini katika mifumo ya ikolojia ya Serengeti, Tarangire - Manyara, Moyowosi - Kigosi, Burigi - Chato na Hifadhi ya Taifa Saadani.

***Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki***

40. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya Mwaka 1998, kuendelea na mapitio ya Sheria ya Misitu Sura 323 na Sheria iliyoanzisha TAFORI Sura 270. Aidha, Wizara kupitia TFS itaanzisha shamba jipya la miti lenye ukubwa wa hekta 3,000 katika Wilaya ya Nzega na kuongeza hifadhi nne za misitu ya asili zenye hekta 37,000 katika wilaya za Babati na Simanjiro. Vilevile, Wizara itapandisha hadhi misitu 10 ya hifadhi yenye ukubwa wa hekta 25,862 kuwa misitu ya hifadhi ya mazingira asilia; kukarabati njia za kutembea watalii zenye urefu wa kilometa 355; na kuanzisha kampuni tanzu itakayosimamia miradi ya kuongeza thamani na kuzalisha bidhaa mseto za mazao ya misitu na nyuki.

**Sekta Ndogo ya Utalii**

41. **Mheshimwa Spika,** Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Utalii ya mwaka 2008 na kuandaa Programu ya Taifa ya Uendelezaji Utalii; na kuendelea kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora wa nyota. Pamoja na hatua hizo, Wizara kupitia TTB itaendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kushiriki maonesho ya utalii katika masoko ya kimkakati. Aidha, TTB itaendelea kutangaza mazao mapya ya utalii ikiwa ni pamoja na utalii wa fukwe, utalii wa mikutano, utalii wa utamaduni, utalii wa meli na kadhalika.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** juhudi mbalimbali za kutangaza utalii zitafanyika kupitia maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa yakiwemo S!TE, Kili/Karibu *Fair,* Karibu Utalii Kusini, GLITE na *East Africa Trade Fair*. Katika kuimarisha utoaji wa mafunzo ya utalii nchini, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii utaanzisha kampasi mpya yaMwanza na programu ya mafunzo ya utalii katika ngazi ya cheti kampasi ya Arusha.

**Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale**

43. ***Mheshimiwa Spika,***Wizara pamoja na kazi nyingine itafanya tathmini ya hali ya uhifadhi wa maeneo matano ya malikale; upimaji wa mipaka ya vituo vitano vya mambo ya kale; na kuratibu maadhimisho ya Tamasha la Mwezi wa Urithi wa Utamaduni, Kumbukizi ya Vita vya Majimaji na Siku ya Kimondo Duniani. Aidha, Wizara kupitia Shirika la Makumbusho ya Taifa litajenga Onesho la Historia ya Tanzania kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, wakati wa harakati za kudai uhuru na Tanzania ikiwa huru. Vilevile, Shirika litakusanya taarifa za kihistoria za Marais ili kuanzisha Makumbusho ya Marais itakayojengwa Dodoma.

**Miradi ya Maendeleo**

44. ***Mheshimiwa Spika,***katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara itatekeleza miradi sita ya maendeleo ambayo ni: Mradi wa Kuendeleza Utalii Ukanda wa Kusini (REGROW); Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili; Mradi wa Kuzuia na Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara;Mradi wa Panda Miti Kibiashara; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki; na Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu (FORVAC).

45. ***Mheshimiwa Spika,***maelezo ya kina ya maeneo mengine kuhusu Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ni kama ilivyooneshwa **kuanzia Aya 116 hadi 156 ya Kitabu cha Hotuba**.

## F. SHUKRANI

46. ***Mheshimiwa Spika,***mafanikio katikautekelezaji wa majukumu ya Wizara yametokana na ushirikiano wake na nchi mbalimbali, mashirika, taasisi na marafiki wa uhifadhi. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau na washirika wa maendeleo kwa kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Korea Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi ni pamoja na AfDB, AWF, AWHF, EU, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF.

## G. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/2021, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe **Shilingi 114,593,952,000** kwa matumizi ya **Fungu 69** - Wizara ya Maliasili na Utalii. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 69,573,850,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi45,020,102,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha **Shilingi 50,852,545,000** za mishahara (PE) na **Shilingi 18,721,305,000** za matumizi mengineyo (OC). Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha **Shilingi 700,000,000** fedha za ndani na **Shilingi 44,320,102,000** fedha za nje.

## H. HITIMISHO

49. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: **www.maliasili.go.tz**.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.



MSAMI WEE ACHA,
MAPENZI KITU KINGINE!
Uk.13

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI MEI 9, 2020




## JOTO HASIRA

# Nicole, Sarah sasa vita kamili

VITA imepamba moto kati ya mke wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize na mpambaji wa video ya wimbo wake mpya wa Bedroom, kiasi ambacho sasa wanaviziana kuonyeshana ubabe.

Mrembo Nicole Joy, ambaye amefanya vizuri katika video hiyo, amemkabili mke wa msanii huyo, Sarah, akimwambia awe makini vinginevyo atamng'oa pua.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Nikole, aliweka ujumbe ambao unasomeka "We sanamu la Michellin nitang'oa hiyo pua'"

Tukio hilo limekuja baada ya kuwapo na msuguano mkali kati ya warembo hao wawili, wakati Harmonize, akiongea na mashabiki wake zaidi ya 5000, kupitia Instagram mubashara.

Wakati msanii huyo akiwa mubashara, aliamua kuwaalika baadhi ya wasanii wengine kuzungumza na mashabiki, akiwamo Nicole Joy na nwigizaji Jacqueline Wolper.

Mashabiki hao walifurahi jambo hilo, wengi wao walitoa maoni kwamba Harmonize na Wolper, wanapendeza na ikiwezekana warudishe mapenzi yao.

Hata hivyo, mashabiki wengine walionekana kushangaa tukio hilo, huku wakihoji kwa nini msanii huyo awasiliane na mpenzi wake wa zamani wakati ana mke wake Sarah.

Harmonize akiwa katika mchezo huo wa hatari, alimpigia simu mrembo Nicole Joy Berry, na kuruka naye hewani huku mashabiki wakipata mihemuko ya kutaka kujua kuna nini kitatokea.

Wakati Nicole na Harmonize wakiwa mubashara, ghafla mkewe Sarah aliibuka na kutuma ujumbe wenye utata akimtaka hapo haitoshi, bali aende nyumbani kwa Nicole akamsalimie.

"Baby nenda salimia Nicole nyumbani" ujumbe huo ulisema na kusababisha mashabiki kushtuka.

Baada ya ujumbe huo, Nicole alijibu kwa haraka kwamba kwamba amuache kwani hana haja ya Harmonize

"Sasa Sarah anaanza kuongea maneno mabaya, unaona comment yake eti nenda salimia Nicole nyumbani, simuhitaji Harmonize nyumbani kwangu na sijampigia mwanamume wako, yeye ndiyo amenipigia, mimi sipendi haya mambo anaanza kuleta habari gani, kwaheri nikibaki hapa mambo yatakuwa mengi".

Baada ya Nicole kusema maneno hayo, mashabiki walizidi kujadili suala hilo na wengine wakimlaumu Hamonize wakisema joto hilo amelitaka mwenyewe kwanini awasiliane na watu ambao wanaonekana ni hatari katika ndoa yake.

BASI SAWA

## TBway ulionja chungu ya mama kijacho

MTANGAZAJI wa shoo ya 5Selekt ya EATV, TBway 360, amesema anahitaji tuzo za kumvumilia mpenzi wake Kim Nana kipindi cha ujauzito wake, kwani alikutana na changamoto nyingi na aliweza kuzishinda.

"Kim Nana siyo Slay Queen, nilianza naye uhusiano muda mrefu sana kama miaka mitano au sita iliyopita, kabla hata ya Instagram haijapamba moto au kuwa na kiki, tulipanga kuwa na mtoto, muda ulipofika tulifanya hivyo japo mwanzoni tulikuwa tunaogopa" amesema T-Bway.

Aidha ameendelea kusema "Kama kuna mwamba aliyevumilia kipindi cha ujauzito basi ni mimi, kuna usiku mmoja alinipigia simu anataka Pizza nikamwambia namtuma mtu au watu wa "Delivery" walete akakataa hadi nikampelekea mwenyewe ila cha ajabu naamka asubuhi hakula hata moja".





## Najma kweli mapenzi sawa na tiba

MREMBO Najdattani, amemkingia kifua mpenzi wake ambaye ni mwanamuziki Barakah The Prince, akisema sasa amebadilika na hawezi kuwajibu vibaya katika mtandao ya kijamii.

Najdattani amesema hayo baada ya mashabiki kulalamika kuhusu tabia ya Barakah, kuwa ndiye msanii anayeongoza kuwajibu mbovu mashabiki mitandaoni.

"Ukweli amelifanyia kazi hilo jambo, sidhani kama kipindi cha hapa karibuni amemjibu mtu vibaya, kuna muda inatokea kama binadamu, kuna ujumbe unakukwaza sana hadi ukapoteza muelekeo, huyu sio Barakah yule ambaye mmemzoea kwamba kila kitu kinamkasirisha ndiyo maana amejitafuta kwenye hiyo miaka miwili". Amesema.





## Hee! Kumbe Jux, Wolper walitoka kimapenzi

MKALI wa muziki wa taratibu wa RnB, Jux, ametoa siri kwamba kumbe alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwigizaji Jacqueline Wolper.

Akizungumza na eNewz ya ETV, Jux amesema kitendo cha kuachana vibaya kuliwafanya kila mtu awe na mambo yake.

"Kipindi cha nyuma nilikuwa naye, inategemea uhusiano unapoishiaga kutokana na mazoea, kwa upande wangu haikuwa sawa sana, lakini nilielewa kutokana na maisha baadaye kila kitu kikawa sawa. Sasa hivi tuko poa, yeye ana maisha yake na mimi nina maisha yangu, hatuna tatizo lolote ni vya muda sana hivi". Amesema Jux





# MASTAA waliomrudia Mungu

SUALA la wasanii mbalimbali duniani kutangaza kuachana na mambo ya kidunia na kuamua kumrudia Muumba wao si geni masikioni mwa watu.

Mastaa wengi baada ya kupata umaarufu kwenye fani zao, baadhi yao wanaamua kuachana na mambo hayo na kuokoka, au kumrudia Mungu na kubadili tabia zao.

Wakati mwingine husababisha majonzi kwa mashabiki wake, lakini furaha kwa watu wanaotaka watu wamfuate Mungu, lakini hili linabaki suala binafsi la mtu mwenyewe.

Hapa nchini kuna baadhi ya wasanii na wanamuziki waliokuwa mastaa, kabla ya kuachana na fani yao na kuamua kumrudia Mungu.

## Msami wee acha, mapenzi kitu kingine!


MSANII wa Bongo Fleva, Msami Baby, amesema ameamua kuachana na mapenzi na kwamba mpenzi wake wa zamani Jacky Cliff, aliachana naye muda mrefu.

Akizungumza na EATV, Msami alisema malalamiko ya mwanamke huyo ni kama njia ya kutafuta kiki na hawezi kusumbuka nayo.

"Yule mdada kiukweli namfahamu ila alikuwa anatafuta engo tu kwa sababu yeye ndiyo alifanya ile interview, kulitokea kukosa maelewano kati yetu kwa hiyo ndiyo akaamua kuja na ishu ile lakini sikupita naye" amesema Msami Baby.



## USIKU WA JUMANNE
## Mapenzi na ushirikina ni vitu tofauti



**Na Adam Fungamwango**

USIKU wa Jumanne ni filamu safi yenye mafunzo ambayo yako kwenye dhana za kishirikina. Filamu hii inaonyesha jinsi mapenzi na ushirikina ni vitu viwili tofauti.

Huwezi kuvichanganya kwa wakati mmoja. Dada mmoja anayeitwa Shija, anaolewa na jamaa, lakini ana kitu kingine tofauti na ndoa ambacho anatakiwa kufanya kwa maagizo ya mama yake.

Usiku mmoja, Mapunda anafiwa na baba yake. Wiki moja baadaye, Jumanne iliyofuata, anafiwa na mama yake. Hii inamchanganya yeye na dada zake wawili, akiwamo Annie.

Annie anajiongeza. Kwa nini baba alifariki Jumanne, mama Jumanne, lakini pia kwenye uchunguzi wake mdogo akagundua kuwa wifi yake Shija huwa halali nyumbani pale siku ya Jumanne.

Anamdokeza kaka yake Mapunda. Naye anakwenda ukweni kwenda kushitaki kuwa mkewe huwa anaondoka siku ya Jumanne, akidai anakwenda kwao.

Mama mkwe anamwambia ni kweli huwa anakwenda kulala pale na si kwamba anachepuka.

Akadai kuwa kuna vitu fulani kwenye mila zao walikiuka, hivyo Shija kila Jumanne anatakiwa kuendelea kuja kulala kwao na si kwa mumewe.

Hali inaendelea kuwa mbaya, kwani Annie anadokezwa kuwa wifi yake Shija ni mshirikina akishirikiana na mama yake na hao ndiyo waliowaua wazazi wao na huko mbele watawaua wote waliobaki ili wachukue mali na hilo ndilo lengo lao.


Annie anaipata siri hiyo kwa mmoja wa ndugu ya Shija ambaye hapendi mambo yanayofanywa na ndugu zake hao.

Lakini pia anampa mbinu za kukabiliana na hilo, kwani wakichelewa wataanza kufa madada wawili wa Mapunda na yeye awe na mwisho.

Annie kila anapomwambia kaka yake Mapunda kuhusu ubaya ya mkewe, anaambulia lawama na vitisho.

Annie anapewa dawa ya kuwanasa washirikina hao. Za mwizi arobaini. Mama yake Shija ananasa kwenye nyumba ya mkwewe. Hapo ndipo Mapunda na watu wengine wanamuamini Annie ambaye awali alionekana ni kama wanawasingizia,

mama na binti yake Shija wanafukuzwa kwa aibu kwenye nyumba ya kina Mapunda, ambapo pamoja na kuonekana kuwa walikuwa wanafanya ushirikina, lakini pia kuhusishwa na vifo vya wazazi wa Mapunda vilivyotokea usiku ya Jumanne, kwenye wiki zinazofuatana.




# Jaywon hukujua kutoka nje ni kosa?

MWANAMUZIKI Olajuwonlo James, maarufu kama Jaywon, amekamatwa na polisi kwa tuhuma ya kukiuka amri ya kukaa ndani kujikinga na COVID-19.

Kulingana na mtandao wa Punch, mwimbaji huyo alikamatwa na polisi waliokuwa doria baada ya kuonekana yupo nje ya nyumba yake kinyume na kizuizi kilichowekwa na serikali.

Jaywon alifunguliwa mashitaka na idara ya polisi ya makosa ya jinai na anatarajiwa kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma zake.



## DJ Khaled kumbe muoga

RAPA mkali kutoka Marekani, DJ Khaled, amewapiga marufuku wanawake kuacha kujipitisha kwake na nguo zinazoshawishi mapenzi.

Akizungumza na mashabiki wake kupitia Instagram Live, DJ Khaled, ambaye baba wa watoto wawili   HYPERLINK "https://www.pulse.com.gh/entertainment/celebrities/dj-khaled-welcomes-another-one-as-wife-gives-birth-to-their-second-child/k630zjg" \t "_blank" Asahd na  Aalam, haraka aliwatahadharisha mashabiki wake kwamba yeye ameshakuwa baba, hivyo lazima kuwe na staha heshima.

Ombi hilo alilitoa baada ya shabiki mmoja kumtumia picha yenye utata ambayo msanii huyo anaeleza haifai na inaleta hisia kali za kimahaba.

## Clarence ukijinasua chinja kuku

UTATA umeibuka baada ya kukamatwa kwa muongozaji wa video wa Nigeria, Clarence Peter, kufuatia vifo vya ghafla vya mnenguaji na mpambaji wa video za muziki.

Kulingana na msemaji wa polisi wa Logos, msanii huyo bado anachunguzwa kutokana na tukio hilo la kushangaza.

Polisi walimkamata muongozaji wa video wa mwanamuziki huyo,Clarence Peters, kwa ajili kuchunguza vifo vya mnenguaji maarufu,Kodak.





## Gigi umekuwa mama kijacho

HATIMAYE mwanamitindo wa kimataifa,

Gigi Hadid, ameondoa ukimya baada ya kuthibitisha  ana ujauzito.

Gigi amekua kimya baada ya kuibuka fununu kuwa anatarajia kupata mtoto na mchumba wake, Zayn Malik.

"Hakika tungependa kueleza hili tukiwa wote, lakini sote tuna furaha na kusaidiana kwa kila jambo katika muda huu unaohitaji usaidizi," amesema Gigi.

## Rick Ross hukujua kulea ni kazi?

RAPA mkali kutoka Marekani, Rick Ross, amefunguliwa mashitaka ya kushindwa kuwatunza watoto wake wawili.

Mama wa watoto hao, Briana Camille, aliamua kukimbilia mahakamani kudai matunzo ya watoto hao baada ya mwanamuziki huyo kudaiwa kuwatelekeza.

Kulingana na mtandao wa HotNewHipHop, rapa  huyo anatakiwa kumlipa mamilioni ya pesa mwanamke huyo kama gharama ya matunzo ya watoto hao.



MAKALA




Mmoja wa wagonjwa wa corona akipatiwa matibabu katika hospitali moja nchini China. **PICHA: MAKTABA**

## UNYANYAPAA COVID 19

# Afrika inahangaika kupima, kutibu, kuzika waathirika

**Na Mwandishi wetu**

SUALA la unyanyapaa, limekuwa kikwazo katika kukabiliana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu, unaosababishwa na virusi vya corona katika nchi mbalimbali duniani.

Kutokana na hali hiyo, inaelezwa inaweza kuwa vigumu kupata takwimu sahihi ya watu wanaougua au kufa kutokana na ugonjwa huo.

Katika nchi za kiafrika, matukio ya unyanyapaa umekithiri kiasi ambacho watu wanaogopa kwenda hospitali wakihofia kuwekwa karantini.

Hata kwa wale wanaokufa, mazishi yake yanaleta hofu baada ya kuonekana wanazikwa bila kuzingatia utu wa binadamu, hivyo husababisha watu kuwa na wasiwasi kupimwa Covid-19.

Baadhi ya nchi kama Kenya, serikali imekuwa ikilazimisha watu kupimwa kwa lazima na kuleta malalamiko kwa wananchi wake wengi.

Serikali za kaunti nchini humo, zinaelezwa hazitumii busara kukabiliana na wagonjwa wa Covid-19 na familia zao, bali nguvu zinatumia kuwapima watu.

Utumiaji wa nguvu ni chanzo cha kushamiri kwa unyanyapaa na kuleta changamoto za kijamii katika serikali barani Afrika wakati zinapokabiliana na covid-19.

Kutokana na watu kuficha taarifa za afya zao, ni vigumu kufahamu takwimu sahihi za maambukizo mapya, waliokufa au bado wanaogua wakiwa nyumbani.

Wakati kisa cha kwanza cha Covid-19 kilipothibitishwa nchini China, katika baadhi ya sehemu Afrika vitendo vya chuki dhidi ya raia wa China na wenye asili ya Asia vilijitokeza.

Kenya na Ethiopia zilikosolewa kwa kuendelea kutoa huduma za ndege hadi nchini China.

Raia wa Nigeria waliandamana dhidi ya uamuzi wa serikali kuwakaribisha madaktari kutoka China kutoa huduma nchini humo.

Radio Biafra, kituo cha redio cha siri kinachopigania kujitenga kwa eneo la kusini mashariki mwa Nigeria, kilisema China imedhamiria kusambaza ugonjwa huo kote ulimwenguni.

Pia Afrika Kusini ilikosolewa kwa kuwarudisha raia wake zaidi ya 100 kutoka mji wa Wuhan, ambako ni kitovu cha ugonjwa wa Covid-19

Wakati ugonjwa huo unazidi kusambaa katika nchi za Afrika, mgawanyiko umejitokeza kuhusu uhalali wa kutaja majina ya wagonjwa wa corona ili kurahisisha ufuatiliaji wake.

Chama cha wandishi wa habari nchini Ghana, kimeonya kwamba kuweka wazi taarifa za walioathirika kutafanya wawe katika hatari ya kuchukiwa na kunyanyapaliwa.

Nchini Liberia, hoja hiyo ilisababisha mtafaruku kati ya maofisa waandamizi, baada ya mwanamke aliyepatikana na virusi vya corona kujificha kwa hofu ya kunyanyapaliwa.

Mgonjwa mmoja aliyepona ugonjwa wa Covid-19, nchini kenya alianza kudhalilishwa mitandaoni, licha ya vyombo vya habari kumuona kama shujaa.

Wagonjwa na wahudumu wa afya wa Afrika Kusini, wamesema suala la unyanyapaa limeathiri sekta ya afya.

"Wakati huu kama mtu akipona ugonjwa wa Covid-19, bado anapata mfadhaiko, tunahitaji kuwa na washauri ili kupona. Licha ya kunusurika na ugonjwa wenyewe, bado tuna tatizika kiakili," anasema mgonjwa kupitia mtandao wa ENCA.

Mwanamke mmoja alijiua akiwa katika karantini kwenye kituo kimoja cha matibabu magharibi mwa Kenya. Kituo cha habari cha Citizen, kilisema kwamba mwanamke huyo alikuwa akilalamikia mazingira magumu katika kituo cha karantini.

Mwanamuziki mmoja nchini Gabon alisemekana kutoroka kutoka kituo cha afya katika mji huo kwasababu ya kukosa matibabu bora.

"Nimekuwa hopitali kwa siku 10, sikuwahi kupata matibabu yoyote, sikuona haja ya kuendelea kukaa kwenye hospitali hiyo. Hakuna aliyenipa hata dawa ya maumivu." Anasema mwandishi mmoja katika video aliyoisambaza katika mitandao ya kijamii.

Suala la kukosa huduma katika vituo vya afya, limeikumba familia moja nchini Kenya, ambayo inadai kijana wao ambaye alipatikana hana virusi vya corona, alikufa kwa kukosa matibabu katika hospitali moja mjini Mombasa.

Hata hivyo, serikali bado hazijapata suluhisho la namna ya kuzika watu waliofariki kwa corona kalingana na imani za kidini kama inavyotakiwa.

Huko Nigeria, waumini wa Kiislamu wamepokea miongozo kutoka chombo kinachowasimamia, kuhusu namna ya kuzika wapendwa wao bila ya kuathiri wengine,

Hali ni tofauti nchini Ghana, ambako vyumba vya kuhifadhi maiti vimejaa, huku familia zikisubiri ushauri wa serikali kama inawezekana watu kuruhusiwa kuzika wapendwa wao.

"Kawaida mazishi huwa ni jambo kubwa na mara nyingi hufanyika mwishoni mwa wiki. Mazishi hujumuisha kuimba na kucheza, na inaweza kuwa ya gharama kama harusi. Lakini familia haziwezi kuchukua miili ya ndugu zao hadi kanuni ya kutokaribiana itakapolegezwa," Tovuti ya Joy imesema.

# UNHCR na mzigo usioisha wakimbizi nchini Tanzania

Na Mwandishi Wetu



Augustine Mahiga(kushoto), akiwa katika ziara ya kikazi katika kambi ya wakimbizi, alipokuwa mtumishi wa UNHCR.

ILIPOTOKEA watu wasiojulikana walivamia kambi ya wakimbizi Kaskazini mwa Burundi mwaka 1995, jumla ya wakimbizi 50,000 kutoka Rwanda walikimbilia nchi jirani ya Tanzania.

Kilichotokea baada ya hapo ni mkanganyiko. Badala ya kuwapokea kama ilivyozoeleka kwa Tanzania, ilichukua hatua haraka ya kutunga miaka yake chini ya ulinzi wa askari, wakimbizi hawakukubaliwa kuingia.

Ni zama ambazo nchi tayari ilikuwa na kundi la wakimbizi nusu milioni, ikisema hawa wanatosha. Ilikuwa katika mateso makubwa ya kubeba mzigo huo.

Uamuzi huo ulizua mkanganyiko kuhusiana na ulimwengu wa haki za binadamu. Tanzania inawezekana kuwa miongoni mwa nchi masikini sana kiuchumi na hata kwa kipindi chote kabla kufikia uamuzi huo wa mpakani utokanao na kutoridhishwa, imekuwa ikikubalika sana kimataifa kwa mwelekeo wake.

Aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, mwaka 1983 alitunukiwa medali maalum na Shirika la Umoja wa Matatifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), kutokana na nchi yake kuwapa uraia wakimbizi wote wa kudumu, pamoja na ardhi. Maelfu walipokea.

Sera ya kuwapokea na kuwalinda wakimbizi tangu ilipopata uhuru wake, iliundwa na mjumuiko wa maslahi ya nyumbani na kimataifa, ikiwamo suala la ukombozi Kusini mwa Afrika; mshikamano wa bara (Afrika) na sera ya nyumbani Ujamaa na Kujitegemea nchini Tanzania.

Wakati wakimbizi wa Burundi na Rwanda walipokewa kwa misingi ya ubinadamu, wale waliokimbia harakati za ukombozi walijikita zaidi katika mtazamo wa kuhikamana kisiasa na wanaoonewa.

UKARIMU & KERO

Ilipotimu wakati harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika na vita vya wenyewe nchini Msumbiji, zimefikia mwisho wake, Tanzania ilijiona sasa wema wake umezawadiwa.

Hata hivyo, katika upande mwingine suluhisho la kinachojiri katika nchi za Rwanda na Burundi, ikawa ngumu kudhibiti, pale inapoona wimbi la wakimbizi wanazidi na kuchochea kero isiyoisha nchini.

Itikadi ya kijamaa iliwajengea Watanzania wema wa kiasili walinao Waafrika, kuwapokea waliokimbizwa makwao, waishi kujisikia kwa misingi ya haki kamili.

Mtumishi wa UNHCR, Yefime Zarjevski, ameandika katika kitabu chake kinachojadili Ujamaa kiitwacho 'Future Preserved'(baadaye umehifadhiwa) akifafanua kwamba imani iliyopo, utajiri wa nchi uko katika watu wake, kauli aliyomrejea Nyerere hata ilipotolewa alipewa tunu ya UNHRC.

Hii ilianza kubadilika katika miaka ya 1990, pale siasa za vyama vingi na uchumi wa soko na mambo huria, ziliikandamiza Ujamaa na siasa ya chama kimoja.

Viongozi wa kisiasa na vikundi vya upinzani walianza kuongezeka nchini Tanzania, wakipinga sera za kuwafungulia milango wakimbizi nchini, huku ardhi ya nchi nayo ikipanda thamani maradufu.

Hapo hapo, mwaka 1994 kuna wastani wa wakimbizi 500,000 walioingia Tanzania wakitokea Rwanda, walikokimbia mauaji ya kimbari.

Tanzania ilielemewa na mzigo wa wakimbizi, huku majasusi na wauaji wakijichanganya na wakimbizi hao halali. Amri na sheria katika kambi za wakimbizi kwa haraka zilipungua nguvu .

Idadi ya wakimbizi nchini nayo iliongezeka mna kuwaelemea wenyeji, kwa wastani katika kila raia watatu wa Kitanzania (waliko wakimbizi), alikuwepo mkimbizi mmoja. Wananchi walishuhudia kero za misitu kuteketezwa, pia mito na ardhi nzuri kuharibiwa.

Kimsingi, kuwasili wakimbizi wa Rwanda kulibadili maisha ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, hata ikashinikiza mageuzi ya kisera nchini Tanzania, ilichofanya katika mpaka wake, kama ishara wazi ya mageuzi rasmi mwaka 1995.

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani wakati huo, Emmanuel Mwambulukutu, alieleza mwelekeo mpya wa nchi kwamba:"Kuhifadhi wakimbizi kumekuwa mzigo mzito na unaouma, kuliko zama zilizopita kwa nchi zinazohifadhi wakimbizi kama Tanzania.

"Kuwalinda na kuwasaidia wakimbizi, imeleta hatari mpya kwa usalama wa taifa, kuibua mvutano kati ya mataifa na uharibifu mkubwa wa mazingira."

Alibainisha kwamba mvutano uliibuka kati ya Tanzania na Burundi kuhusu suala la wakimbizi na namna Tanzania haiko tayari kuruhusu kuzorota usalama wake, kwa sababu kuna mabaya yaliyofanyika Mashariki ya Zaire (Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo-DRC), kwa chanzo cha wakimbizi.

Nyumbani (Naibu Waziri Mwambulukutu) alisema, Watanzania wametawaliwa na hofu kwa sababu ya kuwapo wakimbizi wengi na hata kuna hatari ya raia kuingia katika msuguano na wenyeji, au wasikubaliane kutafuta majibu sahihi'

Wakati sera kama hizo zikionyesha ishara 'kuchoshwa kwa nchi mwenyeji', hata hivyo Tanzania iliendelea kutamka itaendelea kuheshimu wajibu wa kibinadamu. Hadi sasa (1997) Tanzania ina wastani wa wakimbizi 330,000, kiwango kikubwa kuliko nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Ni muhimu kwamba, wajibu wa nchi usiachwe ukatelekezwa, kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali za kusaidia nchi hizo zinazowahifadhi na kudhibiti madhara yatokanayo na wakimbizi.

Jumuiya za kimataifa zinapaswa kujihusisha zaidi na mataifa ya kikanda, katika kushughulikia mzizi wa matatizo ya kuwapo wakimbizi, hata kama inahusisha juhudi za kutatua vita vya wenyewe.

Sera ya UNHCR ni kukusanya rasilimali kwa ajili ya kusaidia maeneo wanakoathirika wakimbizi na raia wenyeji wanapaswa kuhusishwa katika mipango yote, kwa chochote kipya kinachoibuka.

Katika Tanzania, hii imegharimu Dola za Marekani milioni saba (zaidi ya Sh.bilioni 16) na nchi nyingine na UNHCR inahimiza usaidizi wa pamoja, katika kupanua mipango ya haki za binadamu.

Ni muhimu kuonyeshwa kwamba, kanuni za haki za binadamu zinaendana na maslahi rasmi ya nchi. Pia, ni mambo yanayoenda mbali zaidi ya ukusanyaji rasilimali, ikijumuisha mashauriano ya kila mara kati ya serikali na mashirika ya haki za binadamu.

Mchakato wa mabadiliko ya kidemokrasia katika nchi kama Tanzania, inapaswa kutoa fursa ya ujenzi wa misingi ya haki za binadamu, ikiwamo hifadhi ya wakimbizi.

Hata hivyo, hotuba ya Waziri Mwambulukutu na utashi wake, unapaswa kutambuliwa hata kwa nchi nyinginezo zinazohifadhi idadi kubwa ya wakimbizi kwa kiwango kinachofanana.

Ulikuwa mshale, kati ya upinde wa jumuiya za kimataifa, zikikumbushwa kwamba, uongozi umebadilika na hakuna mbadala rahisi uliobaki.

- **Ni tafsiri isiyo rasmi ya makala iliyochapishwa kutoka jarida la UNHCR liitwalo 'Refugee Magazine' Desemba, mwaka 1997, wakati huo Marehemu Augustine Mahiga, alikuwa Naibu Mkurugenzi wa UNHCR, anayeshughulikia Maziwa Makuu, kutoka ofisi ya Geneva, Uswisi.**



Kambi mojawapo la wakimbizi iliyoko Kigoma, Tanzania na pilika zake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**.

# Miaka 15 jela kwa kumuua ndugu yake

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Kigoma imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Kajana, Wilaya ya Buhigwe, Doto Simoni (21), kifungo cha miaka 15 jela baada ya kukiri kumuua bila kukusudia ndugu yake Manase Ezekieli kwa kumpiga na mti usoni na kufariki dunia papo hapo.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji wa Mahakama hiyo, Athumani Matuma baada ya mshitakiwa huyo kukiri kosa.

Matuma alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali kwa mshitakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa vijana wengine wenye tabia za kikatili kama yake.

Alisema mshitakiwa alimuita Manase ambaye kwa sasa ni marehemu aliyekuwa akiishi Wilaya ya Kasulu amfuate kwa ajili ya kumpa dawa ili asilogwe na wachawi.

Jaji Matuma alisema alipofika, mshitakiwa alimchukua ndugu yake huyo na kumpeleka kando ya mto Chai na kumwambia akae chini na kufumba macho na kisha anyanyue uso juu, ndipo alipochukua mti na kumpiga usoni kitendo kilichomfanya aanguke chini na kufariki dunia papo hapo.

Vile vile, alisema mshitakiwa alirudi nyumbani kwake na kunyamaza kimya na kudai kuwa hajui ndugu yake alipo.

Alisema ndugu wengine wa marehemu waliendea kutoa taarifa polisi za kupotea kwa ndugu yao na walianza kumtafuta sehemu mbali mbali.

Alisema ndugu wengine wa marehemu pamoja na polisi walimshuku mshitakiwa na kumkamata na kumbana ndipo alipokiri kumuua.

Jaji Matuma alisema baada ya kufika eneo la tukio, walikuta mifupa ya binadamu za nguo za marehemu ambazo ni shati, suruali, bukta na mti, ambazo ndugu wa marehemu walizitambua kuwa ni za marehemu Ezekiel.

Jaji Matuma alisema kitendo alichokifanya mshitakiwa huyu ni cha kikatili pamoja na kukiri kosa lake mahakama inamtia hatiani kwa kosa la kuua ndugu yake bila kukusudia.

Alisema upande wa mashitaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Benedict Kivuma.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili wa kujitegemea Diana Damson, uliiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa bado mdogo na amekaa mahabusu kwa miaka miwili.

Hata hivyo, Jaji Matuma alitupilia mbali utetezi huo.

Awali akisoma hati ya Mashitaka Wakili wa Serikali Kivuma alidai hapo mahakamani kuwa Januari 15, mwaka 2018 majira ya mchana katika Kijiji cha Kajana, mshitakiwa alimuua ndugu yake kwa kumpiga na mti usoni na kuanguka chini na kufariki dunia.



Mbunge wa Liwale mkoani Lindi, Zuberi Kuchauka (kulia), akisalimiana na Katibu wa Afya wa Wilaya ya Liwale, Maneno Kitinde, kwa staili ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona, mjini humo juzi, kabla ya kumkabidhi gari la kubebea wagonjwa ambalo ni miongoni mwa magari 50 ambayo Waziri Mkuu KassimMajaliwa, aliyekabidhi kwa baadhi ya wabunge hivi karibuni. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mbunge alia uhaba wa walimu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalumu, Alfredina Kahigi (CUF), ameitaka serikali kuangalia upya mgawanyo wa walimu unaofanywa kwenye shule za msingi na sekondari kwa kuwa baadhi ya shule za mijini zinakuwa na walimu wengi huku za vijijini zikitelekezwa na kuwa na upungufu mkubwa wa wataalamu hao.

Amesema hali hiyo imekuwa ikichangia kuzorota kwa utoaji elimu hasa kwa shule za vijijini, akitolea mfano katika mkoa wa Kagera ambao una upungufu mkubwa wa walimu wa masomo ya sayansi kwa shule za sekondari na upungufu wa walimu wa masomo karibu yote kwa shule za msingi.

Akizungumza jijini Dodoma jana, Kahigi alisema wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka ujao wa fedha, alifikisha kilio hicho bungeni kwa kutaka hatua za haraka zichukuliwe kwa kuwa hali ni mbaya hasa katika mkoa huo.

Kahigi aliitaka serikali kuingilia kati ili kulipatia ufumbuzi tatizo hilo, akibainisha kuwa Mkoa wa Kagera pekee, una upungufu wa walimu wa sekondari wa sayansi 435 huku msingi kukiwa na upungufu wa walimu 6,925.

Mbunge huyo pia alishauri wajenge nyuma za walimu, walimu waongezewe shahiki zao, akisisitiza kuna haja mwalimu wa kijijini akumbukwe kwa fedha za kumwezesha kufuatilia huduma makao makuu ya wilaya, anatumia fedha nyingi muda mwingi safarini.

Hivyo, aliiomba serikali kuboresha mazingira ya utoaji huduma za elimu nchini kwa kuongeza nyumba za walimu pamoja na kuboresha maslahi yao ili waendelee kutoa huduma bora ya elimu kwa watoto.

Mbunge huyo pia aliitaka serikali kuongeza mishahara kwa walimu, akibainisha kuwa wako baadhi ya walimu wamefundisha kwa muda mrefu bila kupandishwa madaraja na bila kuongezwa mishahara.

# Walalamika upelelezi kuchukua siku 526

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili rais wa zamani wa migodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu, Deogratius Mwanyika na wenzake, umedai kuiandikia mahakama barua kulalamikia upelelezi kuchukua siku 526 bila kukamilika.

Kadhalika utetezi uliomba mahakama imweleze Mkurugenzi wa Mashitaka Nchini (DPP), arejeshe majibu kiofisi kuhusu malalamiko ya upelelezi kuchelewa kukamilika.

Wakili wa utetezi, Hudson Ndusyepo, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Godfrey Isaya, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Awali, Wakili wa Serikali, Esther Martin, alidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kwamba kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa.

Mbali na kumlalamikia upelelezi washtakiwa kupitia Mahakama ya Mtandao, waliomba kuonana na mawakili wao ili wajadiliane kuhusu mwenendo wa kesi yao.

Mahakama ilikubali ombi la washitakiwa na imeamuru washitakiwa waletwe mahakamani Mei 22, mwaka huu.

Pia, mahakamani imeagiza Wakili wa Serikali kuwasiliana na mamlaka ya juu ili tarehe iliyopangwa wawasilishe majibu.

Mwanyika na wenzake wanakabiliwa na mashitaka 39, likiwamo la kutakatisha fedha na kukwepa kodi zaidi ya Dola za Marekani milioni 112.

Washitakiwa wengine ni Meneja Uhusiano wa Mgodi wa Bulyanhulu, Alex Lugendo, Mkurugenzi Mtendaji wa Pongea, North Mara na Bulyanhulu Assa Mwaipopo, kampuni ya Mgodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu.

Washitakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza Oktoba 17, 2018.

Katika kesi ya msingi, washitakiwa wanakabiliwa na mashitaka matatu ya kula njama, mashitaka saba ya kughushi, 17 ya utakatishaji wa fedha, kuwasilisha nyaraka za uongo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuongoza uhalifu wa kupangwa, mashitaka nane ya kukwepa kodi na moja la kutoa rushwa.

Washitakiwa wanadaiwa, kutenda makosa hayo kati ya Aprili 11, 2008 na Juni 30, 2007 katika sehemu tofauti za jiji la Dar es Salaam, Kahama mkoani Shinyanga, Tarime Mara, Biharamulo Kagera maeneo ambayo yapo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.
Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

# Mauaji Harusini-11

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




Baada ya ziara ya nyumba yake aliyoiacha mwaka mmoja uliopita na kuona kila kitu kiko sawa, aliamua ajipumzishe kutokana na safari ndefu ya zaidi ya masaa 24.

Alijua siku tatu baada ya kutua nchini anatakiwa kwenda kuripoti ofisini. Alitaka kuzitumia siku tatu hizi kuwasiliana na kukutana na ndugu zake, kabla hajaanza kazi. Anajua kabisa kuwa kazi zao huwa haziaminiki.

Kingine kilichomjia kichwani ni kwenda kuzuru kaburi la shangazi yake.

"Ndiyo. Kabla ya kuanza kazi nitakwenda kuzuru kwenye kaburi la shangazi." Aliwaza.

Kifo cha shangazi yake kilimkuta wakati akiwa nchini Marekani akimalizia mitihani yake.

Aliumia mno, kwa sababu alikuwa ni wa mwisho kuzaliwa kutoka kwenye ukoo wa baba yake.

Alikuwa mmoja wa shangazi zake ambaye anaelewana naye sana. Labda kwa sababu wote walikuwa vijana.

Hata hivyo kilichomuuma zaidi ni jinsi alivyokufa. Pamoja na kwamba kifo ni lazima binadamu na mwanadamu aliyezaliwa ipo siku atakufa, lakini kifo cha shangazi yake kilimshangaza na kumshtusha kwa wakati mmoja.

Kitu kimoja tu ambacho kilikuwa kwenye akili yake ni kwamba shangazi yake hakufa kifo cha kawaida. Haikuwa mapenzi ya Mungu.

********************************

Gari aina ya Toyota Brevis ilisimama kwenye mti mkubwa, kando tu ya barabara ya Kinondoni, inayounganisha barabara ya Salenda na barabara ya Kawawa.

Ilikuwa sehemu za Kinondoni Makaburini. Eddy Kamal aliteremka ndani ya gari hilo akiwa peke yake. Alivaa suruali nyeusi na shati jeusi, viatu pia vyeusi kuashiria msiba. Ramani aliyopewa haikukosewa, alikwenda moja kwa moja kwenye kaburi lililokusudiwa.

Macho yake yalielea kwenye msalaba uliokuwa umewekwa nakshi, huku kukiwa na jina Grace Maumba.

Naam. Hilo ndilo kaburi alikuwa akilihitaji. Lilikuwa ni la shangazi yake.

Alifika na kupiga magoti. Akafumba macho. Kaomba na kusali kwa dakika kadhaa. Alipomaliza akasimama.

"Shangazi umekufa kifo cha kikatili. Umekufa kifo ambacho hukustahili. Ucheshi wako, tabia yako jinsi ilivyo haikustahiki ufe kifo kibaya kama hiki. Pamoja na mambo mengine, nitahakikisha namtioa mbaroni yoyote yule aliye nyuma ya mpango huu na wenzake pia." Alijisemea kimoyomoyo.

Kilikuwa kiapo. Kiapo alichokiweka Eddy mbele ya kaburi la shangazi yake Grace.

Aligeuka kichwa chake kulia. Macho yake yalikutana na kiumbe. Kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi, Eddy alihisi kusisimkwa na kitu mwilini.

Alijihisi kama ndani ya moyo na mwili wake haukuwa kawaida kwa muda huo.

Aliyemuona ni msichana. Kwa kumkadiria hakuwa amevuka hata miaka 25. Alikuwa amepiga magoti kwenye kaburi ambalo nalo lilionekana lina umri kama la shangazi yake Patiyo.

Cha kushangaza zaidi ni kwamba rangi na staili ya ujenzi wa kaburi alilokuwa yule msichana lilifanana sana na la shangazi yake.

Alikuwa amevaa gauni jeusi, lakini nje akiwa amevaa khanga, juu akiwa amefunga pia kilemba cheusi.

Alionekana na majonzi. Ingawa yeye tayari alikuwa amemaliza taratibu zote. Lakini akili yake yote ikamuangazia msichana na kaburi alilokuwa anasali.

Ilipita kama dakika 10 hivi, msichana akawa amemaliza sala yake. Alijizoazoa akiwa peke yake na kuanza kuondoka taratibu. Hakufikisha hatua tano, Eddy alikuwa ameshafika karibu naye.

"Habari yako bibie." Eddy alimsalimia huku macho yake yakifanya ziara fupi kwenye sura ya msichana huyo aliyeonekana mrembo, licha ya kwamba alikuwa amevaa kimsiba zaidi.

Sekunde kadhaa zilipita, msichana huyo akimkodolea macho Eddy. Ni kama vile alikuwa anafikiria kama alishawahi kumuona hata siku moja, lakini hakupata jibu.

"Sijambo." Alijibu kwa kifupi.

"Vipi, mbona uko peke yako hapa. Msichana mdogo kama wewe, ulitakiwa uwe hata na ndugu zako au watu wa kukuleta sehemu kama hii, huogopi?"

Msichana alimtazama tena Eddy, akamjibu "Mimi leo ndiyo nimepata nafasi, ndugu zangu walikuja jana."

"Ni kaburi la nani yako?"

"Baba mzazi."

"Pole sana mama." Eddy alimpa pole na kumgusa begani.

"Ahsante nishapoa." Alijibu msichana huyo ambaye naye sauti yake ilianza kuwa ya chini na upole zaidi.

"Mbona naona kama siku aliyofariki baba yako ndiyo na mimi siku aliyofariki ndugu yangu kwenye kaburi lake hapa."

Msichana aliinua macho na kumtazama kwa makini Eddy, huku akitazama kidole chake kilipoelekezwa.

Ndipo msichana huyo aliposhtuka, kwani kaburi alilolionyesha jamaa aliyekuwa naye hapo ni la mke wa baba yake, ambao waliuawa pamoja, masaa machache tu baada ya harusi.

Alichoona Eddy ni machozi ya msichana huyo kutiririka badala ya jibu. Kama mwanaume alijua jukumu lake.

Alimkumbatia na kuanza kumbembeleza. "Usilie mama, au kuna kitu nimekosea?"

"Kwani we hujui? Kwani we hujui?" Alilia kwa kwikwi mtoto wa watu.

"Sijui. Mimi ninachojua hilo nilokuonyesha ni kaburi la shangazi yangu."

"Hawezi kuwa shangazi yako, wakati hujui nini kilitokea." Msichana alizidi kulia.

"Najua. Ila kuna mengine siwezi kujua kwa sababu sikuwepo nchini."

Jibu hilo lilimfanya msichana huyo anyamaze kidogo na kumuangalia kwa makini mwanaume aliyemkumbatia kimbembeleza wakiwa wawili tu kaburini, majira ya saa nne asubuhi.

"Ni kwamba, mimi nilikuwa nchini Marekani. Nikiwa huko nilipata taarifa kuwa shangazi yangu ameuawa. Lakini kuuawa kwake aliuawa pamoja na mwanaume mmoja aliyefunga naye ndoa. Mimi huyo mwanaume simjui, sijawahi kumuona, lakini nimeambiwa kuwa waliuawa wakiwa wametoka kufunga ndoa." Eddy alijibu, jibu ambalo kidogo lilionekana kama kumfariji msichana huyo.

"Basi huyu baba yangu ndiye alikuwa mume wa huyo aliyekuwa kwenye kaburi hilo ulilonionyesha." Msichana alijibu na kuanza kulia tena.

"Baba yako ndiyo mume wa shangazi yangu?" Eddy aliuliza.

"Kama ndiyo unayemsema huyo aliyezikwa kwenye kaburi hilo Grace Maumba ni shangazi yako, basi ndiye aliyekuwa mke wa baba yangu mzazi na ndiyo waliouawa wote wakitoka kufunga ndoa." Bado Msichana huyo alikuwa akielezea akilia kwa kwikwi.

"Wewe mwenyewe unaitwa nani?"

"Naitwa Shani."

***Itaendelea Jumamosi***

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO



**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**IDDI JUMA MTATURU**
anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P0938/0715 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MBEZI BEACH HIGH SCHOOL mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MS/RB/9136/2016.**

157360

## MNADA WA HADHARA

ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPLIES T. LTD & COURT BROKER MNADA WA HADHARA UTAFANYIKA TAREHE 23/05/2020 SAA 4: ASUBUHI, KWA IDHINI YA MAHAKAMA YA MWANZO YA DODOMA MJINI KESI NAMBA 234 YA MWAKA 2019.

TUTAUZA NYUMBA ILIYOPO MTAA WA LIVING LIFE SCHOOL KUFIDIA DENI ANALODAIWA.

**MAWASILIANO PIGA NO. 0713913150.**

157361

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

MWL WYNN ANYOSISYE MWANGOKA AMEPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI T 655 BXF CANTER MITSUBISHI. CHASSIS NO. FE537EV52D674.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

**TAARIFA YA POLISI: MBE/TUK/R-B/356826/2020.**

157356

## JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo …….Hai …..Kati……………………..
Usimamizi wa Mirathi namba,…..02….mwaka 2020
Ombi la Rehema Aikande Kiwera kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu Meselemia Alelyo Mushi
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa Kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo ….10…/06/….2020………kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe…….. 06 -05-……….mwaka 2020

SAHIHI YA HAKIMU

157358

## KADI YA GARI IMEPOTEA

DANIEL PROTASY CHALLE anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.618 BES aina ya TOYOTA VISTA. Yenye chasis namba SV500007661 na Engine namba 3S7551066.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

TAARIFA POLISI: TAN/RB/360998/2020.

157357


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# MBAPPE
## MFUNGAJI BORA LIGUE 1

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amethibitishwa kuwa mshindi wa kiatu cha dhahabu kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kwa msimu 2019-20 kwa kuibuka mfungaji bora baada ya ligi hiyo kufutwa.

Wiki iliyopita, Ligi Kuu Ufaransa ilifutwa rasmi kwa msimu huu baada ya mamlaka ya serikali kusema kwamba hakutakuwa na matukio yoyote ya michezo hadi Septemba mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Klabu ya Paris Saint-Germain ilipewa ubingwa kwa kwa sababu ilikuwa ikiongoza kwa pointi 12 kileleni mwa msimamo dhidi ya Marseille ambao wamemaliza nafasi ya pili.

Mbappe alikuwa akiongoza kwa mabao 18 sawa na mshambuliaji wa Monaco, Wissam Ben Yedder.

Hata hivyo, Ligue 1 imethibitisha kupitia tovuti yake kwamba, Mbappe atatambulika kama mfungaji bora kwa sababu mabao yote alifunga kutokana na uchezaji dimbani, huku Ben Yedder mabao yake matatu yalitokana na penalti.

Uwiano wa mabao wa Mbappe kwa mchezo pia ulikuwa bora, kwani mabao hayo 18 alifunga katika mechi 20, huku Ben Yedder alifunga katika mechi 25.

Mshambuliaji wa Lyon, Moussa Dembele, amemaliza nafasi ya tatu akiwa na mabao 16.

## DYBALA ATAMANI POGBA ARUDI JUVE

**TURIN, Italia**

PAULO Dybala ana matumaini ya kucheza tena pamoja na mchezaji mwenzake wa zamani wa Juventus, Paul Pogba kwa siku za usoni.

Fowadi huyo wa Argentina, Dybala, alicheza pamoja na Pogba kwa msimu mmoja kabla ya kiungo huyo kuondoka kwa Bianconeri hao na kurudi Manchester United mwaka 2016.

Pogba amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa mara ya pili pale Old Trafford kwa msimu ya hivi karibuni.

Real Madrid imekuwa ikimtaka mshindi huyo wa Kombe la Dunia, huku nayo Juve pia ikionyesha nia ya kutaka kumrudisha.

Dybala angependa kuona usajili huo unakamilia wakati akielezea uhusiano wake mzuri na Pogba katika mahojiano na Uefa.com.

"Ningependa kucheza naye tena," amesema Dybala.

"Paul ni rafiki yangu, ambaye napenda kucheza nae kwa sababu ni mchezaji mzuri na anayenivutia.

"Nina matumaini siku zijazo nitacheza nae tena hapa, nina uhakika atarudi kuja hapa na tutacheza tena wote."

# Rakitic hafikirii kuondoka Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

IVAN Rakitic amesisitiza "anafuraha sana" pale Barcelona na haupi uzito uvumi kwamba anataka kuondoka, wakati huu akijiandaa kumaliza mkataba wake hapo Camp Nou.

Kiungo Rakitic mkataba wake wa sasa unamalizika Juni mwaka 2021, lakini amekuwa akihisishwa na kuondoka kwa Blaugrana hao.

Nyota huyo wa kimataifa wa Croatia alikuwa akitajwa kwamba anaweza kutumika kama chambo kwa Neymar kuondoka Paris Saint-Germain, huku pia klabu ya Sevilla ikiripotiwa kumwania.

Lakini Rakitic mwenyewe amesema anapenda kucheza hapo Barca na maisha yake ameyatoa kwa vinara hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

"Napenda maisha ya hapa," alisema akiiambia Sky Sport. "Nimekuwa hapa kwa miaka sita sasa, hivyo nipo hapa na napapenda.

Rakitic alijiunga na Barca akitokea Sevilla katika msimu wa 2014-15 na alimaliza msimu huo kwa bao kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Juventus na aliisaidia Barca kutwaa mataji manne ya LaLiga.

HABARI MICHEZO




# NEYMAR
## SASA ATABAKIA PSG

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR bado atabakia Paris Saint-Germain msimu ujao, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake, Leandro Paredes.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil ameripotiwa kuwaniwa na Barcelona, ambapo aliondoka kule na kutua PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222 Agosti, mwaka 2017, na ameripotiwa kuwa tayari kupunguziwa mshahara ili arudi pale Camp Nou.

Neymar amefunga mabao 69 katika mechi 80 alizocheza kwenye mashindano yote kwa PSG msimu huu.

Msimu wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, umefutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, huku timu hiyo ya kocha, Thomas Tuchel ikipewa ubingwa ikiwa ni kwa mara ya nne mfululizo, na Paredes anatarajia kuona Neymar anabakia kwenye klabu hiyo kwa msimu wa 2020/21.

"Neymar atabakia na sisi," amesema Paredes akiiambia FOX Sports Argentina.

"Naamini atakuwa hapa na ataendelea kucheza hapa PSG, ingawa anaweza kufanya uamuzi wake."

# Klose atajwa kocha msaidizi wa Bayern

**MUNICH, Ujerumani**

MIROSLAV Klose ametajwa kuwa kocha mpya msaidizi wa Bayern Munich inayonolewana Hansi Flick.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Ujerumani amesaini mkataba wa mwaka mmoja na ataanza kazi rasmi Julai Mosi, mwaka huu.

Msaidizi wa sasa wa Flick, Danny Rohl mkataba wake unamalizika Juni 30, mwaka 2023.

"Hansi Flick na mimi tunajuana vizuri tangu tukiwa pamoja kwenye Timu ya Taifa ya Ujerumani, tunaaminiana na tunaelewana," amesema Klose, ambaye amekuwa kocha wa kikosi cha Bayern cha umri chini ya miaka 17 kwa miaka miwili.

"Kwa upande wangu, hii ni hatua nzuri katika maisha yangu ya ukocha. Natumaini kwa uzoefu wangu naweza kutoa mchango muhimu kwa Bayern kutimiza malengo yake."

Klose, ambaye alistaafu soka mwaka 2016, alishinda mataji mawili ya Bundesliga na mawili ya DFB-Pokal kwa miaka minne aliyokaa na Bayern.

Amecheza mechi 137 kwa Timu ya Taifa na kufunga mabao 71, ambapo alitinga fainali ya Kombe la Dunia, mwaka 2002 na Euro 2008, kabla ya kushinda Kombe la Dunia mwaka 2014.



# Mkhitaryan hataki kubakia Roma




**ROME, Italia**

HENRIKH Mkhitaryan hajatuma ujumbe kwa Arsenal kuwajulisha kwamba ana mpango wa kubakia Roma moja kwa moja, wakala wake, Mino Raiola amesema.

Mkhitaryan, raia wa Armenia, alijiunga na Roma kwa mkopo na amechangia mabao sita na asisti nne katika mechi 17 alizocheza.

Kwa mujibu wa ripoti ya gazeti la Corriere dello Sport la Jumatano, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ameiambia Arsenal anataka kubakia nchini Italia na ana matumaini kwamba watafikia makubaliano na Giallorossi hao.

Hata hivyo, Raiola amekanusha madai hayo kwa kusema kwamba mteja wake hajasema hivyo.


"Mkhitaryan hajatuma ujumbe kwa Arsenal," Raiola aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Kwa hakika kabisa hizi ni taarifa za uzushi kabisa na hazikubaliki."

Kocha wa Roma, Paulo Fonseca na nahodha Edin Dzeko awali walibainisha kwamba wangependa Mkhitaryan apewe mkataba wa kudumu.

Mkhitaryan alijiunga na Arsenal kutoka Manchester United kwa dili lililomhusisha Alexis Sanchez kwenda upande mwingine Januari 2018.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA AFUNGUKA 'ALIVYOLIMISI' SOKA

Kiungo huyo Mfaransa asema anasubiri kwa hamu kurejea dimbani baada ya...

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, anafurahia kurudi kucheza soka baada ya kuwa nje ya dimba tangu Desemba kutokana na majeruhi na kusimama kwa msimu kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa corona.

Ligi Kuu England bado imesimama kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.

Wakati Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, inatarajia kuanza Mei 16, mwaka huu, majadiliano kuhusu kurudi kwa Ligi Kuu England bado yanaendelea, huku Ligi Kuu Ufaransa maarufu Ligue 1, na ile ya Uholanzi, Eredivisie, tayari zikiwa zimefutwa.

Pogba alikaribia kurudi dimbani wakati msimu uliposimamishwa Machi, mwaka huu akiwa amecheza mechi sita tu kwa United msimu huu, na mshindi huyo wa Kombe la Dunia anasubiria kwa hamu kurudi dimbani.

"Kwa hakika nimelikumbuka soka," amesema Pogba akimwambia mbunifu wa mavazi, Stella McCartney katika mahojiano kwenye makala ya kampuni ya vifaa vya michezo ya Adidas.

"Niliumia, hivyo nilikuwa nafanya mazoezi peke yangu kwa zaidi ya miezi saba, wakati najiandaa kurudi uwanjani ukatokea mlipuko wa virusi vya corona, hivyo tukaacha kila kitu.

"Nataka kurudi tena uwanjani. Nimekosa mechi nyingi, na nataka kuwa bora kabisa. Hivyo wakati nitakaporudi uwanjani natakiwa kuwa kwenye ubora wangu."

Pogba amemwambia McCartney amekuwa akijifua mwenyewe kipindi hiki ambacho wamezuiliwa kutoka ndani.

"Nimekuwa nyumbani na nikijifua mwenyewe. Nimetengeneza uwanja mdogo nyumbani, uwanja wa soka na naweza kufanya mazoezi nikicheza na mwanangu wa kiume, tunacheza wote," amesema.

## KWA UFUPI

**NEWCASTLE KUMSAJILI COUTINHO**

NEWCASTLE United itatumia kiasi cha pauni milioni 70 ili kumsajili kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho, kama wamiliki wapya watafanikiwa kuinunua klabu hiyo. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 yuko kwa mkopo Bayern Munich. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**KOULIBALY KUTUA NEWCASTLE**

MABOSI wapya wa Newcastle wameweka wazi nia ya kumsajili beki wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly. Beki huyo mwenye umri wa miaka 28 anatarajia kuondoka katika klabu hiyo ya Italia katika majira ya joto kwa dau la pauni milioni 69.8. ***(Sky Sports via Star)***

**DORTMUND YAJIAMINI**

BORUSSIA Dortmund inatarajia kuona winga wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 20, anabakia klabuni hapo licha ya kutakiwa na Manchester United. ***(Sky Sports)***

**ICARDI ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL inapewa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Mauro Icardi (27), kama mrithi wa straika wake raia wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang. Aubameyang (30), anamaliza mkataba wake mwakani wakati Icardi yeye yuko kwa mkopo Paris St-Germain. ***(Tuttosport, via Teamtalk)***

**LEWIS MAMBO SAFI**

ARSENAL inakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili, George Lewis ambaye ni mchezaji huru. Winga huyo wa Timu ya Taifa ya Norway ambaye ana umri wa miaka 19, kwa sasa yuko katika klabu ya Tromso. ***(Goal, via Metro)***

**GREALISH AKARIBIA UNITED**

MANCHESTER United inaendelea na mchakato wake wa kuwania saini ya kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish (24), ambaye thamani yake kumwondoa klabuni hapo imetajwa kuwa ni pauni milioni 50. ***(Sun)***

**JURADO AITOSA BARCA**

BEKI chipukizi wa Barcelona, Marc Jurado (16), amekataa kusaini mkataba wa vigogo hao wa Hispania na sasa anajiandaa kujiunga na Manchester United katika kipindi cha majira ya joto. ***(ESPN)***

**CHILWELL ATAJWA SPURS**

BEKI wa kushoto wa Leicester City na Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell (23), ni mmoja wa wachezaji muhimu wanaotakiwa na Tottenham Hotspur ambayo Kocha wake Jose Mourinho anajipanga kusuka upya safu yake ya ulinzi. ***(Foot Mercato)***

**MERTENS, NAPOLI SAFI**

NYOTA anayewindwa na Chelsea, Dries Mertens, tayari amefikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na klabu yake ya Napoli. Mshambuliaji huyo Mbelgiji mwenye umri wa miaka 33, anamaliza mkataba wake ifikapo kipindi cha majira ya joto. ***(Calciomercato - in Italian)***

**LIVERPOOL YAMTAKA RASHICA**

WINGA wa Timu ya Taifa ya Kosovo na Wolfsburg, Milot Rashica (23), anatajwa kuwindwa na Liverpool, Rais wa Shirikisho la Soka Kosovo (KFF), amesema.***(Standard)***

**ALLEN KUTUA LEEDS**

VINARA wa Ligi ya Championship, Leeds United, wanapewa nafasi kubwa ya kumsajili kiungo wa Linfield, Charlie Allen (17). Nyota huyo raia wa Ireland Kaskazini pia anawindwa na Chelsea, Tottenham na Liverpool. ***(Yorkshire Post)***

HABARI MICHEZO

# TARIQ AANIKA KIKWAZO KINACHOWATESA YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Tariq Seif, amesema kukosekana kwa uwanja wa mazoezi unaomilikiwa na klabu hiyo, ni moja ya changamoto inayowakabili wachezaji wa timu hiyo tofauti na wenzao walioko katika kikosi cha Simba na Azam FC.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Tariq alisema endapo Yanga itafanikiwa kupata uwanja wake, wachezaji watasikia furaha na programu zao za mazoezi zitafanyika kikamilifu.

"Kitendo cha kutokuwa na uwanja binafsi wa mazoezi au kuchezea mechi ni changamoto kwetu, lakini tukiwa na uwanja wetu tutafarijika," alisema Tariq.

Mshambuliaji huyo alisema kwa sasa anaendelea vizuri na mazoezi kwa kufuata maelekezo waliyopewa na Kocha Mkuu, Luc Eymael ili kuwaweka sawa tayari kumazilia msimu wa 2019/20 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema kwa upande wake ametumia vema kipindi cha mapumziko kujiimarisha ili Ligi Kuu itakaporejea atimize malengo ya kuisaidia timu yao kupata mafanikio.

"Lengo langu ni kuipa mafanikio Yanga, nitajituma kwa nguvu zangu zote nitakapokuwa uwanjani, nitafurahi kuona tunamaliza ligi tukiwa kwenye nafasi za juu kwenye msimamo," Tariq alisema.

Nyota huyo amewataka wachezaji wenzake kuendelea kufanya mazoezi kwa bidii huku wakijikinga na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona kama inavyoshauriwa na wataalamu wa afya.

"Nafanya mazoezi huku nakijikinga na ugonjwa wa corona, kila mmoja asiupuuze, ni ugonjwa wa kuogopwa na watu wote," mshambuliaji huyo alisema.

Hadi Ligi Kuu Bara inasimama, Yanga yenye pointi 51 baada ya kucheza mechi 27, iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo nyuma ya Azam FC yenye pointi 54 huku vinara wakiwa ni Simba wenye pointi 71.

## Cheka kugombea Urais wa ngumi

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA maarufu wa ngumi za kulipwa nchini, Francis Cheka, ametangaza kuwania nafasi ya Urais katika uchaguzi mdogo wa Chama cha Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC).

Akizungumza na gazeti hili jana, Cheka, alisema amechukua uamuzi wa kuwania uongozi kwa sababu anaufahamu vema mchezo huo ambao umewahi kulitangaza vizuri jina la Tanzania.

Cheka alisema anaona anafaa kuchaguliwa katika nafasi hiyo kutokana na kuzijua changamoto wanazokutana nazo mabondia wanapokuwa katika mapambano mbalimbali ndani na nje ya nchi.

"Ninaujua vema mchezo wa ngumi, fitina zake, changamoto zake, mazuri yake na maumivu yake kama bondia ambaye nimecheza ngumi kwa muda mrefu," alisema Cheka.

Bondia huyo aliongeza yuko katika mchezo huo tangu mwaka 1999, hivyo hakuna jambo asilolijua linalohusiana na ngumi.

TPBC inalazimika kufanya uchaguzi mwingine kutokana na viongozi waliochaguliwa katika uchaguzi uliofanyika mwaka jana kujiuzulu kwa sababu mbalimbali.




Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi akifanya mazoezi kwa mara ya kwanza jana akijiandaa na mechi za LaLiga ambayo inatarajiwa kurejea hivi karibuni. **PICHA: MAIL**

## Judo yaandaa katiba mpya

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mchezo wa Judo Tanzania (JATA), kimesema kimeanza kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wa mchezo huo, kwa ajili ya kurekebisha katiba ya chama hicho, imeelezwa.

Katibu Mkuu wa JATA, Innocent Mallya aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana mchakato huo utasaidia kuandaa katiba mpya na wanaamini hautachukua muda kwa sababu ya kushirikisha wadau wao.

Mallya alisema wadau hao ndio walioanzisha mchakato huo na wanaamini watakitendea haki chama hicho kwa kushiriki kikamilifu kwenye zoezi hilo.

**"Chama chetu kilianzishwa tangu mwaka 2002, tumekuwa tukitumia katiba ambayo iliandaliwa wakati huo hadi sasa, tumeona ni muda sahihi wa kuifanyia marekebisho, haikuwahi kufanyiwa mabadiliko ya aina yoyote," Mallya alisema.**

Kiongozi huyo alisema viongozi wa ngazi ya mikoa watapokea maoni na kuyawasilisha kwenye uongozi wa Taifa na baada ya hapo watayafanyia kazi kama malengo yao yalivyowekwa.

"Kama michezo ikiruhusiwa, basi tutakuwa na kikao mwezi ujao, kikao ambacho kitakuwa na mjadala mkubwa kuhusiana na katiba na tutawashirikisha wadau mbalimbali," alisema Mallya.

Aliwataka wadau hao kutumia muda huu wa karantini kuwasilisha maoni ya katiba ili viongozi wa juu wayafanyie kazi na michezo itakaporejea waendelee na maandalizi ya mashindano mbalimbali.

"Kwa sasa mchezo wetu umekuwa na mvuto wa aina yake baada ya watu wengi kujiunga, imekuwa tofauti na miaka mingine," aliongeza.

# Klabu Ligi Kuu mambo magumu

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imezitaka klabu zote nchini kuendelea kusaka wadhamini na kujipanga ili kukamilisha msimu wa Ligi Kuu Bara 2019/20, endapo utarejea.

Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili, Ligi Kuu ya Wanawake na mashindano ya Kombe la FA, yalisimamishwa na serikali ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Mwenyekiti wa TPLB, Stephen Mguto, alisema bodi hiyo fedha wanazopokea kutoka kwa wadhamini hazitoshi, hivyo hawana uwezo wa kuzipatia klabu hizo kama zinavyowaomba.

"Tungependa kuona tunazisaidia klabu zetu, lakini hali haituruhusu, tunachopokea kutoka kwa wadhamini hakitoshi, hapa tulipo tunamadeni ya waamuzi hatujawalipa, kusema kweli bado udhamini ni mdogo," alisema Mguto.

Aliongeza hata kabla ya janga la corona, klabu zilikuwa na bajeti finyu, lakini zilipambana kuhakikisha zinaandaa timu na zinamaliza msimu.

Michezo
Jumamosi Mei 9, 2020
Nipashe



## Pogba afunguka 'alivyolimisi' soka

HABARI UK 22



Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela ambaye amezungumzia mipango ya klabu hiyo ya jijini Dar es Salaam kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: MAKTABA**

## Kipingu aelezea inapokwama Stars

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Kanali Mstaafu Iddi Kipingu amesema kutokuwapo kwa taasisi mahususi zilizoundwa kwa ajili ya kuendeleza vipaji vya wanamichezo hapa nchini ni sababu mojawapo ya kushindwa kutoa wachezaji nyota.

Kipingu aliliambia gazeti hili jana kuwa, wachezaji chipukizi na wenye vipaji wa hapa nchini wameshindwa kutimiza ndoto zao kwa sababu ya kukosa ushirikiano kutoka katika jamii inayowazunguka.

**Alisema baadhi ya wachezaji waliolelewa katika Shule ya Sekondari Makongo akiwamo Boniface Pawasa na Juma Kaseja, walipata nafasi ya kuendelezwa baada ya kusajiliwa na Simba na kuitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).**

"Tukitaka kufanya haki iliyo haki, kila mtu, kila kikundi kinatakiwa kujua wajibu wake katika kuendeleza vipaji, katika kuendeleza watoto hawa," alisema Kipingu.

Alisema Tanzania haina sera ambayo inamlazimisha kila mmoja kutekeleza wajibu wake na sera ambayo ilikuwapo miaka ya nyuma haikutendewa haki.

Alisema hapo awali wazazi walikuwa wakifuatilia zaidi maendeleo ya darasani na kutotaka kufahamu maendeleo yake kwa upande wa michezo au sanaa tofauti na baadhi ambao wameanza kufuatilia.

# YANGA YAANZISHA MPANGO KAZI

### Lengo ni kukamilisha mikakati ya usajili wa wachezaji nyota Afrika ambao wanatarajia...

**Na Saada Akida**

ILI kurejea kwenye ushindani katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa msimu ujao, uongozi wa Yanga umesema umeandaa 'mpango kazi' utakaohakikisha wanakamilisha kwa asilimia 100 usajili wa wachezaji wenye viwango vya juu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema klabu hiyo iko katika hatua nzuri ya kukamilisha mazungumzo ya kumsajili mchezaji nyota ambaye atasaidia timu yao kutimiza malengo yake kwenye msimu ujao.

Mwakalebela alisema ujio wa mchezaji utachangia kuleta mabadiliko na mapinduzi kwenye soka la Tanzania na uongozi wa Yanga unataka kuona wanafanikiwa kukamilisha mpango hiyo.

"Tumepanga kufanya usajili mkubwa kwa ajili ya msimu ujao, mchezaji ambaye atasaini 'dili' jipya na Yanga atakuwa ni mwenye hadhi ambayo haijawahi kutokea kwenye Ligi Kuu, lengo ni kuwa na kikosi tishio," alisema Mwakalebela.

Kiongozi huyo alisema wameongeza umakini baada ya kubaini changamoto walizokumbana nao katika msimu huu na wanajua kufanya vema kwa timu hiyo, ndiyo furaha pekee inayosubiriwa na wanachama na mashabiki wao.

"Mwaka huu kutakuwa na tofauti kubwa ya mwaka jana, tutakuja na mpango tofauti kabisa kuhakikisha tunashusha majembe, na hii itasaidia jezi zetu kuuzika sana, hasa za wachezaji wapya ambao tutakuwa tumewaleta," Mwakalebela alisema.

Aliongeza deni walilonalo viongozi wa Yanga ni kufanya usajili mzuri na hiyo ni ahadi yao kwa mashabiki na wapenzi wa klabu yao baada ya kutokuwa na msimu mzuri mwaka huu.

"Katika jambo ambalo limejenga hasira kichwani mwetu ni kukosa ubingwa misimu mitatu, hivyo tumeona upungufu wetu, na kuhakikisha tunayafanyia kazi ikiwamo usajili," alisema Mwakalebela.

Baadhi ya wachezaji ambao wanatajwa kuwindwa na Yanga ni pamoja na kiungo wa Timu ya Taifa ya Rwanda (Amavubi) na Rayon Sports, Ally Niyonzima, Yidah Sven, Reliants Lusajo na Bakari Mwamnyeto.

Wakati huo huo mabosi wa Mtibwa Sugar, wamesema hawana mpango wa kuwaruhusu nyota wao wawili, Abdulhalim Humoud na Salim Kihimbwa, ambao wanatajwa kuwindwa na Yanga kwa ajili ya msimu ujao.

Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru alisema uamuzi wa kutowauza wachezaji hao unatokana na nyota hao kuhitajika katika kikosi cha timu hiyo.

"Nyota hao ni miongoni mwa moyo wa timu yetu, hivyo hatujafikiria kwa sasa kuwaruhusu kirahisi rahisi, licha ya kujivunia klabu yetu ni chuo cha kuibua vipaji," alisema Kifaru.

Aliongeza Homud na Kihimbwa wana mkataba ya kuitumikia Mtibwa Sugar hadi mwaka 2022 na wanaamini msimu ujao wataisaidia timu hiyo kurejea kwenye ushindani.

"Ukiangalia kwa upande wa Humoud, bado yuko katika mipango yetu kwa ajili ya msimu ujao, hatuna mpango wa kumwacha, wanapambana kuhakikisha wanaendelea kusaidia timu yetu," alisema msemaji huyo.

Licha ya kutokuwa na msimu mzuri mwaka huu, mapema Januari timu hiyo ilitwaa ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar baada ya kuifunga Simba bao 1-0.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >